*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo

**Netanyahu** aapa kuendeleza vita dhidi ya **Hamas**



Uk. 19

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00067 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Mei 29 - Juni 4, 2024 |

# Dk. Samia kuimarisha sauti ya Tanzania UN

■ **Lengo kurejesha heshima ya nchi katika anga za kimataifa**

Uk. 4



"Tutahakikisha tunapiga kura kimkakati na kuongozwa na Sera ya kutofungamana na upande wowote.

**4R**

Balozi za Tanzania nje ya nchi, zimepewa jukumu la kuielezea na kuitolea ufafanuzi.



## Vipaumbele tisa Elimu Zanzibar

Uk. 4



## Mazingira wezeshi ya kuwainua wanawake kiuchumi ni muhimu

Uk. 16



## Hedhi salama kwa ustawi...

Uk. 14



## Naona dalili za wapinzani wengi kuja CCM 2025

Uk. 12

## Kazi pevu za Rais zinavyowaumbua wanafiki

Uk. 15







SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI MHE. LELA MUHAMED MUSSA (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

## Mei, 2024

***UTANGULIZI***

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liingie katika Kamati ili niweze kutoa maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema tukaweza kukutana tena katika kikao hiki cha kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Aidha, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukamilisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na tukaweza kusherehekea Sikukuu ya Eid-el-Fitr kwa salama na amani. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie kheri na baraka zake na aniwezeshe kuwasilisha hotuba hii kwa ufasaha mkubwa na awajaalie wasaa wajumbe wote wa baraza hili kuichangia vizuri na hatimae waweze kuipitisha kwa kauli moja.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuipa kipaumbele sekta ya Elimu iliyotupelekea sote kushuhudia mabadiliko makubwa ya elimu ndani ya kipindi kifupi. Maamuzi haya ya Serikali yametuwezesha kutekeleza maazimio mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kwa kiwango kikubwa tukaweza kufikia shabaha zilizowekwa zikiwemo za Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambazo kwa upande wa elimu tayari tumevuka shabaha kwa maeneo mengi. Aidha, Nichukuwe Fursa hii pia kumshukuru Mama Maryam Mwinyi, Mke wa Rais wa Zanzibar kwa mashirikiano na ukaribu anaotupa katika kuimarisha elimu Zanzibar.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** Jitihada hizo za Serikali zina mchango mkubwa katika kuhakikisha upatikanaji wa fursa sawa ya elimu bora kwa wote sambamba na kuzalisha wataalamu wa fani mbalimbali ambao watalisaidia Taifa kwa kuliletea maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa na hatimaye kufikia malengo ya Taifa ya Dira 2050 ya kuifikisha Nchi yetu katika Uchumi wa kati wa Juu. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie afya njema, hekma, busara na maarifa zaidi Rais wetu Dk. Hussein Ali mwinyi, ili aendelee kutuongoza vizuri. Pia napenda kutoa pongezi zetu na shukurani za dhati kwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa utendaji wao mzuri na kumpa mashirikiano ya karibu Mheshimiwa Rais.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa dhati kabisa nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha umoja wa Watanzania, amani na mshikamano ulioimarisha mashirikianao baina ya sehemu zote mbili za Muungano. Jitihada hizo zimesaidia sana kufanya kazi kwa kujiamini na kutujengea uwezo uliopelekea kutatua changamoto zetu nyingi zikiwemo udhamini wa wanafunzi wa elimu ya juu.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Pia nichukue fursa hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili na kusimamia mijadala na hoja za Wajumbe katika kuchangia mipango na mikakati ya Serikali yenye kuchochea maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishieni busara, hekima, umahiri na uadilifu katika kutekeleza majukumu yenu. Aidha, nichukuwe fursa hii kumshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Niwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii wakiongozwa na Mwenyekiti wao shupavu Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani kwa kuwa karibu sana nasi na kutupa mashirikiano na maelekezo ambayo matokeo yake yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha sekta ya elimu nchini. Aidha, niwashukuru Wenyeviti na wajumbe wote wa Kamati zako mbali mbali. Pia niwashukuru sana wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao na michango yao wanayoitoa kwa maendeleo ya nchi yetu.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** Niwashukuru kwa dhati kabisa watendaji wote wa "Presidential Delivery Beureu" (PDB) Chini ya Mtendaji Mkuu wao Prof. Mohammed Hafidh Khalfan, kwa mashirikiano wanayoendelea kutupatia katika maeneo mbalimbali yaliyosaidia utekelezaji wa Miradi ya Mikakati hasa ujenzi wa skuli. PDB pia walitusaidia kwa kiasi kikubwa katika kuratibu na kusimamia uwekezaji binafsi kwenye sekta ya elimu mfano wawekezaji wa kampuni ya ROK kutoka Uturuki waliojenga Skuli kubwa ya Kisasa eneo la Fuoni, na pia kushirikiana na Tony Blaire Institute katika kuwajengea uwezo watendaji wa WEMA kupitia mfumo wa Priority Project Results Agreement (PPRA).

9. ***Mheshimiwa Spika,*** Nichukuwe fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Ali Abdulghulam Hussein kwa kunipa mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii. Pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Utawala, Naibu Katibu Mkuu Taaluma, Afisa Mdhamini wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi mbali mbali za Elimu, Maafisa wa ngazi mbalimbali wa Wizara, bila kusahau walimu na Kamati zetu za skuli kwa mashirikiano yao makubwa katika kuleta maendeleo ya elimu nchini. Aidha, shukurani ziwafikie wazazi, wanafunzi na wadau wote wa elimu wa ndani na nje ya nchi kwa ushiriki na michango yao katika kusaidia harakati za utoaji na upatikanaji wa huduma ya elimu iliyo bora kwa wote. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa imani na uzalendo kwa nchi yetu.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwisho nawashukuru sana watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Tume ya Mipango, Ofisi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, ZAECA na Ofisi ya Mufti

*Inaendelea uk. 3*

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Mkuu wa Zanzibar na Taasisi nyengine kwa ushirikiano wao ambao umechangia katika kuimarisha huduma za elimu katika mwaka 2023/2024. Ni matumaini yetu kuwa ushirikiano huo utaimarika zaidi katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za elimu bora katika Taifa letu.

11. ***Mheshimiwa Spika***, Utekelezaji wa mpango wa elimu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umetokana na mchango mkubwa na mashirikiano yaliyojengeka kwa muda mrefu kati ya Serikali, Wananchi na Wahisani katika kuchangia utekelezaji wa malengo ya kitaifa.

12. ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya kuelezea matarajio ya bajeti ya mwaka 2024/2025, nitawasilisha utekelezaji wa mpango wa elimu kwa Mwaka wa fedha wa 2023/2024.

***MIRADI YA SEKTA YA ELIMU***

13. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilitekeleza kazi zake kupitia miradi mikuu mitano kama ifuatayo: -

(i) Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu
(ii) Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi
(iii) Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari
(iv) Uimarishaji wa Elimu ya Juu
(v) Uimarishaji wa Elimu ya Amali

***UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024***

14. ***Mheshimiwa Spika***, sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 kupitia programu sita za elimu kama zifuatazo:

**Programu 1:** Elimu ya Maandalizi na Msingi
**Programu 2:** Elimu ya Sekondari
**Programu 3:** Elimu ya Juu
**Programu 4:** Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali
**Programu 5**: Ubora wa Elimu
**Programu 6**: Uongozi na Utawala

***UTEKELEZAJI WA MPANGO WA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024***

15. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mpango wa elimu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umezingatia Programu kuu sita zinazoakisi malengo ya maendeleo ya elimu ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, vipaumbele vya sekta, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

16. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hizo zote zilitekelezwa kwa mashirikiano makubwa kati ya Serikali, Jamii na Washirika wa Maendeleo wa ndani na nje ya Zanzibar. Programu hizi zilitengewa jumla ya **TSh. 457,299,603,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 276,228,600,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, zikiwemo **TSh. 221,464,600,000** za malipo ya mishahara na **TSh. 54,764,000,000** za matumizi mengineyo. Aidha, **TSh. 181,071,003,000** kwa kazi za maendeleo zikiwemo **TSh. 98,970,736,000** kutoka SMZ na **TSh. 82,100,267,000** kutoka kwa Wahisani wa maendeleo.

17. ***Mheshimiwa Spika***, Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 340,226,661,543** sawa na asilimia **74** ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh. 195,978,750,827** sawa na asilimia **88.6** zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **TSh. 28,378,212,823** sawa na asilimia **51.8** zimetumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 115,869,697,893** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh.99,803,098,430** sawa na asilimia **101** ni kutoka SMZ na **TSh.16,066,599,463** sawa na asilimia **20** ni kutoka kwa wahisani ambapo shughuli nyingi za Miradi ya Wahisani zinategemea kukamilika kwa taratibu za Manunuzi zinazoendana na miongozo yao.

18. ***Mheshimiwa Spika***, Utekelezaji halisi kwa kila Programu ni kama ifuatavyo:-

***PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI***

19. ***Mheshimiwa Spika***, Jukumu kuu la Programu hii ni kuimarisha na kutoa elimu ya maandalizi na msingi kwa wanafunzi wenye umri kati ya miaka minne hadi kumi na mbili.

20. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ilitengewa jumla ya TSh. **131,918,709,000** Kati ya fedha hizo **TSh. 95,431,337,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida zikiwemo **TSh. 84,783,251,000** za Mishahara, **TSh. 10,648,086,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 36,487,372,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya **TSh.107,866,938,443** sawa na asilimia **82** zilipatikana.

Shughuli zilizotekelezwa kupitia programu hii na matokeo ya muda mfupi ni Kama inavyoonekana kuanzia ukurasa wa 7 hadi 9.

***PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.***

21. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii inalenga kutoa na kuimarisha elimu ya Sekondari. Jumla ya **TSh. 190,707,359,000** zimepangwa kutumika, kati ya fedha hizo **TSh. 107,410,933,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida zikiwemo **TSh. 93,779,483,000** kwa ajili ya mishahara na **Tsh. 13,631,450,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 83,296,426,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Aprili 2024, jumla ya **TSh. 156,454,334,893** sawa na asilimia **82** zilipatikana. Utekelezaji kwa programu hii na matokeo ya utekelezaji ni kama inavyoonekana kuanzia ukurasa wa 10 hadi 12.

***PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU***

22. ***Mheshimiwa Spika***, Madhumuni ya programu hii ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujiajiri au kuajiriwa. Programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni mafunzo ya ualimu na maeneo manne ya huduma, ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti; Huduma ya Sayansi na Teknolojia; Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu. Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh. 58,724,112,000.** Kati ya fedha hizo, **TSh. 8,929,800,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida zikiwemo **TSh. 22,526,312,000** kwa ajili ya malipo ya mishahara na **TSh. 27,268,000,000** za matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili 2024, Jumla ya **TSh. 42,356,546,499** sawa na asilimia **72** zimepatikana**.** Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

***Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu***

23. ***Mheshimiwa Spika***, Madhumuni makubwa ya Programu hii ni kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mafunzo ya Ualimu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii imepangiwa kutumia jumla ya **TSh. 1,232,612,000.** Kati ya fedha hizo, **TSh. 390,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 842,612,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, Jumla ya **TSh. 868,722,729** sawa na asilimia **70** zimepatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ndogo na matokeo yake ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 13 hadi 14.

***Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti***

24. ***Mheshimiwa Spika***, Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti ina lengo la kuwaandaa wanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira. Huduma hii inatolewa katika Vyuo vikuu vitatu vilivyopo Zanzibar ambavyo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumait na Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU).

25. ***Mheshimiwa Spika***, Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kilitengewa ruzuku ya **TSh. 16,610,400,000** kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya TSh. **15,224,263,244** sawa na asilimia **92** zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo yake ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa 15 hadi 17.

***Huduma ya Sayansi na Teknolojia***

26. ***Mheshimiwa Spika***, huduma ya Sayansi na Teknolojia ni miongoni mwa huduma muhimu katika kuinua kiwango cha Elimu ya Uhandisi, Sayansi na Teknolojia na kuimarisha maendeleo ya uchumi wa nchi. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mwaka 2023/2024, Taasisi hii ilitengewa ruzuku ya **TSh. 9,727,200,000.** Kati ya fedha hizo, **TSh. 7,268,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za Maendeleo na **TSh. 2,459,200,000** ni kwa ajili ya ruzuku ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, Jumla ya Tsh. **2,796,678,299** sawa na asilimia **29** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 17 hadi 19.

***Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu***

27. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar inatekeleza majukumu makuu matatu, ambayo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wenye sifa za kujiunga na masomo ya elimu ya juu; kusimamia na kufuatilia nafasi za ufadhili wa masomo kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo ndani na nje ya Tanzania na kukusanya marejesho ya mikopo ya wanafunzi kutoka kwa wanufaika wote. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya **Tsh. 29,052,900,000** zimetengwa kutekeleza shughuli za huduma hii. Kati ya fedha hizo **Tsh. 9,052,900,000** kwa ajili ruzuku ya kazi za kawaida ikiwemo mishahara na **Tsh. 20,000,000,000** za Maendeleo zilitengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea na masomo ya Elimu ya Juu. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 21,512,117,015** sawa na asilimia **74** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 19 hadi 20.

***Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu***

28. ***Mheshimiwa Spika***, huduma hii ina jukumu la kusimamia na kutathmini maendeleo ya elimu ya juu na inatekelezwa na Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu. Jumla ya wanafunzi 12,306 wakiwemo wanawake 7,468 na wanaume 4,838 wameandikishwa katika vyuo vitatu vilivyopo Zanzibar

*Inaendelea uk. 5*

# Dk. Samia kuimarisha sauti ya Tanzania UN



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imesema imejipanga kuimarisha sauti ya Tanzania katika Umoja wa Mataifa (UN) kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 ili kurejesha heshima ya nchi katika anga za kimataifa.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jijini Dodoma jana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, wakati akisoma hotuba ya bajeti ya wizara hiyo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya mwaka 2024/25. Aliliomba Bunge kupitisha bajeti ya wizara yake ya Sh. bilioni 241.069.

"Tutahakikisha tunapiga kura kimkakati na kuongozwa na Sera ya kutofungamana na upande wowote," alisema na kuongeza:

"Aidha, nchi yetu itaongeza ushiriki katika majukwaa yanayojadili masuala ya kidunia hususani masuala ya kiuchumi, mabadiliko ya tabianchi na matumizi endelevu ya rasilimali."

Alisema Tanzania ni mwanachama katika taasisi, mashirika na jumuiya mbalimbali za kikanda na kimataifa na kwamba uanachama huo una faida mbalimbali kwa nchi ikiwemo za kiuchumi, kiufundi na ushirikiano.

Alisema kupitia uanachama huo, Watanzania wanapata nafasi za ajira katika ngazi za wataalam na uongozi na pia nchi inapata nafasi ya kushiriki kwenye bodi za uongozi za taasisi na mashirika hayo, hivyo kuwa na ushawishi kwenye maamuzi ya kisera yanayopitishwa.

Akizungumzia miaka mitatu ya Rais Dk. Samia madarakani, alisema kumekuwepo na kuimarika kwa ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine na taasisi za kimataifa na upatikanaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania nje.

Alisema katika kipindi hicho, Rais Dk. Samia amefungua nchi na kukuza biashara, uwekezaji na ufunguzi wa balozi mpya katika miji ya Vienna-Austria na Jakarta-Indonesia.

Aidha, alisema kumekuwa na kuongezeka kwa ushawishi na sauti ya Tanzania katika majukwaa ya kikanda na kimataifa pamoja na uteuzi wa Watanzanika katika Jumuiya za Kimataifa na kuongezeka kwa ziara za viongozi wa nje nchini.

Pia alisema mafanikio mengine ni kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco) kutangaza Julai 7 ya kila mwaka, kuwa siku ya Kiswahili Duniani.

Akizungumzia falsafa ya 4R na misingi yake, alisema Balozi za Tanzania nje ya nchi, zimepewa jukumu la kuielezea na kuitolea ufafanuzi na misingi yake wanapotekeleza majukumu yao ya uwakilishi.

Alisema kwa msingi huo, katika kuchangia utekelezaji wa falsafa hiyo inayohimiza Maridhiano (reconciliation), Mageuzi (reforms), Ustahimilivu (resilience) na Kujenga Upya (rebuilding), Wizara inaamini utekelezaji wa suala hili, utaiwezesha jumuiya ya kimataifa kufahamu hatua muhimu zinazochukuliwa na Serikali katika kudumisha demokrasia, haki za binadamu, utawala bora na kulinda tunu za taifa, ikiwemo amani, umoja na mshikamano.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

# Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kutekeleza vipaumbele tisa

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema itaendelea kutekeleza mapendekezo ya ripoti ya mageuzi ya Sekta ya Elimu kwa kutekeleza vipaumbele tisa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alisema hayo wakati akisoma hotuba ya wizara yake kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2024/25 katika Baraza la Wawakilishi mwishoni mwa wiki.

Alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kuimarisha uongozi na usimamizi wa elimu katika ngazi zote za elimu zikiwemo skuli, wilaya, mkoa na wizara na kuimarisha mfumo wa tathmini ya maendeleo ya elimu ya wanafunzi katika ngazi zote za elimu na kupandisha ufaulu wao.

Aidha, kuimarisha miundombinu ya elimu kwa kujenga madarasa 1,500 kupitia ujenzi wa skuli za ghorofa, skuli za chini na kukamilisha madarasa yaliyoanzishwa na wananchi kwa Unguja na Pemba, nyumba 20 za walimu, ofisi ya wizara, ofisi nne za walimu wilaya, vyoo 300, dakhalia nane zikiwemo dakhalia za wanaume za Chwaka Tumbe na Paje Mtule pamoja na kuzifanyia ukarabati mkubwa na mdogo skuli 100 za msingi na sekondari.

Vingine ni kujenga karakana za elimu ya amali katika skuli 33 za Sekondari Unguja na Pemba (karakana tatu kwa kila wilaya) na kujenga uzio katika Skuli ya Sekondari ya Hasnuu Makame na Mohamed Juma Pindua na kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kufundishia na kujifunzia kwa kuziunganisha na Mkonga wa Taifa taasisi za elimu zikiwemo; skuli 217 za sekondari, vituo vya walimu 12 na Vituo vya Ubunifu wa Kisayansi (Hubs) 22 pamoja na kuzipatia vifaa vya Tehama.

Vingine ni kuendelea kutekeleza mtaala mpya wa umahiri kwa elimu ya maandalizi, msingi na sekondari kwa kuwapatia walimu mafunzo na vifaa vya kujifunzia na kufundishia vikiwemo vya watoto wenye mahitaji maalumu, kuimarisha Mafunzo ya Ufundi na Amali kwa kujenga vyuo vitano vya mafunzo ya amali, utanuzi wa Chuo cha Karume (KIST) na ujenzi wa Chuo cha Ubaharia na kuzipatia vifaa.

Vipaumbele vingine ni kuimarisha Elimu ya Juu kwa kuongeza fursa ya upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu Zanzibar kuanzia ngazi ya stashahada; kuanza mradi wa kujenga kampasi ya kudumu ya Chuo cha IIT Madrasa; Ujenzi wa Jengo la Skuli ya kilimo, Jengo la maabara ya sayansi ya kisasa - Suza, Ujenzi wa skuli ya Afya, skuli ya meno na kliniki yake -Suza.

Aidha, alitaja kipaumbele kingine kuwa ni kuimarisha huduma za maktaba kwa kuanza kujenga maktaba mpya ya kisasa pamoja na kuimarisha maktaba mtandao.



# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

ambavyo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumait na Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU). Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kitengo kilitengewa jumla ya **TSh. 70,000,000** kutoka Serikalini. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **Tsh. 53,321,850** sawa na asilimia **76** zimepatikana. Utekelezaji halisi ni kama unavyoonekana kuanzia ukurasa wa 21 hadi 22.

***PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI***

29. ***Mheshimiwa Spika***, programu hii ina madhumuni ya kuwajengea vijana uwezo katika ushindani wa soko la ajira kwa kuwapatia mafunzo ya amali na mbadala. Programu hii ina programu ndogo mbili; Mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala na Watu Wazima. Programu ilitengewa jumla ya **TSh. 37,028,642,302**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 10,044,175,302** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida ikiwemo **TSh. 4,133,075,302** kwa ajili ya malipo ya mishahara, **TSh. 5,911,100,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 26,984,467,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 8,030,057,479** sawa na asilimia **22** zilipatikana.

***Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali***

30. ***Mheshimiwa Spika***, programu hii ndogo ilitengewa jumla ya ruzuku ya **TSh. 35,615,167,000** Kati ya fedha hizo, **TSh. 8,630,700,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida ikiwemo **Tsh. 3,247,600,000** kwa ajili ya mishahara, **TSh. 5,383,100,0000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 26,984,467,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 6,950,070,470** sawa na asilimia **20** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 23 hadi 25.

***Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima***

31. ***Mheshimiwa Spika***, programu hii inatekelezwa na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima na ina lengo la kupunguza kiwango cha wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanajamii. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 1,413,475,302** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **TSh. 885,475,302** ni kwa ajili ya mishahara na **Tsh. 528,000,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 1,079,987,009** sawa na asilimia **76** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii na matokeo ya muda mfupi ni kama ilivyojionesha katika ukurasa wa 26.

***PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU***

32. ***Mheshimiwa Spika***, programu hii ina lengo la kuhakikisha elimu inayotolewa katika ngazi zote inaleta manufaa kwa mwenye kuhitimu, jamii na taifa kwa ujumla. Programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 12,495,809,878**, Kati ya fedha hizo, **TSh 6,075,882,457** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. **6,419,927,421** ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya TSh. **11,415,996,735** sawa na asilimia **91** zilipatikana. Progamu hii ina jumla ya programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama ifuatavyo: -

***Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia***

33. ***Mheshimiwa Spika***, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, Sekondari na mafunzo ya Ualimu. Shughuli za utoaji wa huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Elimu Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Taasisi ilitengewa ruzuku yenye jumla ya **TSh. 1,640,800,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 358,100,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 1,282,700,000** ni kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya **TSh. 1,424,536,753** sawa na asilimia **87** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 27 hadi 29.

***Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu***

34. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utoaji wa elimu. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, huduma ya Upimaji na Tathmini ilitengewa ruzuku ya **TSh. 5,028,100,000.** Kati ya fedha hizo, **TSh. 3,837,200,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 1,190,900,000** ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 5,531,536,883** sawa na asilimia **110** zilipatikana. Ongezeko hili lilitokana na ongezeko la gharama za mitihani ukilinganisha na bajeti iliyotengwa. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 29 hadi 30.

***Huduma ya Ukaguzi wa Elimu***

35. ***Mheshimiwa Spika***, huduma hii ina madhumuni ya kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inafuata sera, sheria, miongozo na taratibu zilizopo. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, huduma hii ilipangiwa jumla ya ruzuku ya **TSh. 2,650,200,000.** Kati ya fedha hizo, **TSh. 487,500,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 2,162,700,000** ni malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya **TSh. 2,006,770,048** sawa na asilimia **76** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 31 hadi 32.

***Huduma za Maktaba***

36. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu, nyaraka na nyenzo nyengine za taaluma kwa watoto, wanafunzi wa ngazi zote na jamii. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023-2024 huduma hii ilipangiwa kutumia ruzuku ya **TSh. 1,065,600,000.** Kati ya fedha hizo **TSh. 741,200,000** ni kwa ajili ya mishahara na **TSh. 324,400,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili 2024 jumla ya **TSh. 804,471,996** sawa na asilimia **75** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha katik ukurasa wa 33.

**Huduma ya Urajisi wa Elimu**

37. ***Mheshimiwa Spika***, huduma hii ina madhumuni ya kuhakikisha sheria, sera na taratibu za Wizara zinafuatwa katika skuli za Serikali na za binafsi. Huduma hii pia inatoa leseni kwa walimu na kuzisajili skuli za Serikali na za binafsi pamoja na vyuo vya ualimu vya kati. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Afisi ya Mrajisi wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, huduma hii ilipangiwa kutumia jumla ya ruzuku ya **TSh. 319,400,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 90,800,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineo na **TSh. 228,600,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 304,517,845** sawa na asilimia **95** zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa 34 hadi 35.

**Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu**

38. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kuifanya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itumike katika ngazi ya utawala, kujifunza na kufundishia, kuimarisha huduma ya mawasiliano na kutunza usalama wa taarifa. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh. 871,065,878**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 300,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 571,065,878** ni kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 521,579,954** ambazo ni sawa na asilimia **60** zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 35 hadi 37.

***Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha***

39. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalum. Programu hii inatekelezwa na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 150,000,000** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya **TSh. 72,819,000** sawa na asilimia **49** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 38 hadi 39.

**Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni**

40. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika elimu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh. 770,644,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 527,882,457** ni kwa matumizi mengineyo na **TSh. 242,761,543** ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 749,764,256** sawa na asilimia **97** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 40 hadi 41.

***PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI***

41. ***Mheshimiwa Spika***, Programu ya Utawala na Uongozi ina lengo la kuhakikisha usimamizi wa matumizi na upatikanaji wa rasilimali bora katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu zikiwemo Programu ndogo ya Uongozi kwa ujumla, Programu ndogo ya shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Elimu Pemba. Programu hii ilipangiwa jumla ya **TSh. 26,424,971,277**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 9,564,682,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, TSh. **9,648,249,277** ni kwa ajili ya mishahara na **TSh. 7,212,040,000** ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 14,102,787,494** sawa na asilimia **53** zilipatikana.

***Programu ndogo ya Uongozi kwa Ujumla***

42. ***Mheshimiwa Spika***, programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha ufanisi wa Uongozi na Utawala wa

*Inaendelea uk. 7*

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

## Tutafutie tiba ya hili

WIKI hii tumeimulika Hospitali Wilaya ya Ilala, Amana katika wodi ya akina mama waliojifungua na kuwa na matatizo haya na yale pale wodi namba 8 kwamba kuna siku wanalala wawili wawili na watoto wao na siku nyingine watatu watatu!

Yaani katika mazingira haya akina mama hawa wazazi, wengine wakiwa na maumivu ya uzazi wanalazimika kupisha watoto wao kitandani kukaa sakafuni.

Hii bila shaka inatokana na wingi wa wagonjwa huku vitanda vikiwa havitoshi. Tulitafutie hili tiba pia kama tunavyotibu hao akina mama.







MAONI YA MHARIRI

## Hatua ya kuboresha elimu, kukuza ujuzi na ubunifu ya kupongezwa

SERIKALI ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imekuwa ikifanya maendeleo na mageuzi muhimu katika elimu. Maendeleo haya hayahusu ujenzi wa madarasa na miundombinu mingine pekee, bali serikali pia imekuwa ikifanya mageuzi kwenye 'mbongo' za vijana wetu.

Hii ni pamoja na utekelezaji wa sera ya elimu na mitaala iliyoboreshwa pamoja na kuendeleza ujuzi na ubunifu. Mpaka sasa kuna shule 96 zenye kibali cha kuendesha elimu ya amali na pia serikali inajenga shule 100 mpya za amali ufundi.

Ni katika muktadha huohuo, hivi tunavyoongea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, inaendesha Wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu pale Tanga iliyoanza Mei 25, 2024 na inatazamiwa kufungwa rasmi Ijumaa ijayo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda anasema maadhimisho ya kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu ni sehemu ya mikakati ya serikali katika kuongeza hamasa ya kukuza elimu ujuzi na ubunifu katika kuchagiza maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Amesema matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ni nyenzo zinazosaidia kutatua changamoto za kiuchumi na kijamii pamoja na kuchagiza maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla.

Waziri Mkenda pia amesema wabunifu nchini wasisite kufika katika wizara na taasisi hususan Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ili bunifu zao ziendelezwe kwani mpaka sasa kuna bunifu zaidi ya 40 ambazo zimeendelezwa na sasa ni bidhaa ziko sokoni.

Tunaipongeza serikali kwa hatua inazochukua katika kufanya mageuzi kwenye elimu yetu ikiwa ni pamoja na kukuza ubunifu.

Tunaamini pia kwamba maonesho ya Tanga yanayoshirikisha zaidi ya washiriki takribani 300 kutoka ndani na nje ya nchi, yataamsha mijadala na kubadilishana uzoefu juu ya masuala ya elimu, ujuzi na ubunifu kwa faida ya Watanzania. Hongera Rais Samia na hongera wizara, kwa kufanya kazi maono ya Rais ya kuhakikisha elimu inakuwa nyenzo hasa ya kukomboa Mtanzania.

Wasiliana nasi

Mhariri Mkuu: +255713263775 / +255748115000
Mhariri wa Habari: +255768411003
Mhariri Michezo: +255784122020
Meneja Masoko/Biashara: +255718480406 / +255733768825
S. L. P: 15110, Dar es Salaam
Makao Makuu Mtaa: Barabara ya Morogoro
Jengo la: Aura Mall
Chumba Cha Habari: +255 (0)222151532
Email: uelekeohabari@gmail.com

Na Hamisi Kibari

JICHO LANGU

## Hakuna namna wamachinga kuondoka barabarani?

WAMACHINGA ni jina walilopewa wafanyabiashara ndogondogo ambao mara nyingi hutembeza bidhaa mbalimbali zikiwa mikononi au kupanga kinyemela kandokando mwa barabara na mitaa ambapo inaaminika kwamba huuza bidhaa hizo kwa urahisi, bila kutoa risiti na kwa bei nafuu kuliko madukani.

Wanaoitwa wamachinga kwa sasa ni vijana wa Kitanzania wanaojiajiri kupitia biashara za mitaji midogo midogo na kukua katika mitaji mikubwa, lakini si wote wanaojiita Wamachinga ni wafanyabiashara wadogo; bali wamo wa kati wanaopitia kivuli cha machinga kufanya biashara zao bila kulipa kodi.

**Ni kweli machinga wanajitafutia riziki lakini lazima kila shughuli iwe na utaratibu.**

Uwepo wa machinga kwa sasa katika maeneo mengi jijini Dar es Salaam hususani mitaa ya Kongo, Msimbazi na maeneo mengine ndiyo kichocheo kikubwa cha wizi wa mali za wafanyabiashara, wizi wa mifukoni kutokana na misongamano kuzidi pamoja na biashara nyingi za magendo kutawala katika maeneo hayo ya biashara kwenye miji husika hapa nchini.

Vilevile uwepo wa Machinga kwenye njia za watembea kwa miguu na kandoni mwa barabara kunachangia kwa kiasi kikubwa foleni za watu na wakati mwingine hata magari na ajali nyingi; bila kusahau uchafuzi wa mazingira kwenye maeneo hayo yanayotakiwa yawe safi nyakati zote.

Kuwepo kwa vijana hao kwenye maeneo hayo kinyemela pia husababisha kero na taabu kubwa kwa watembea kwa miguu, kwani hili la kupanga bidhaa hadi kwenye njia za watembea kwa miguu na hata zile za magari, kamwe haikubaliki lakini wahusika wanafumbia macho kwa kuchelea kuwaudhi baadhi ya wanasiasa.

Cha kushangaza zaidi ni kuwa hata barabara za wendokasi zimejaa vijana hao ambao kwa ujumla wamekaa kila eneo huku wakijua wazi kuwa ni makosa.

Suala la machinga kufanya shughuli bila kufuata taratibu na kanuni limekuwa kero na changamoto kubwa na ya muda mrefu kwa serikali kuu na serikali za mitaa; na matokeo yake imekuwa ikitokea mizozo ya mara kwa mara kati yao na halmashauri za miji, wilaya, manispaa ya majiji pale mgambo wanaposimamia sheria za halmashauri kuhusu usafi na sehemu rasmi za kufanya biashara.

Miongoni mwa sababu kubwa zinazochangia mizozo isiyokwisha kati ya halmashauri na wamachinga ni wanasiasa kuwatumia wafanyabiashara hao kama mtaji wao hususan unapokaribia Uchaguzi Mkuu.

Wanasiasa wengi wanawatumia wamachinga ili kufanikisha malengo yao ya kisiasa, zikiwemo kampeni za uchaguzi na bila kuficha wengi wamefanikiwa katika chaguzi hizo kwa kuwatumia vijana hao.

Kwani nyakati hizo ndipo wanasiasa huwaona wamachinga kuwa bora na muhimu katika kipindi chote hicho cha kampeni.

Wanasiasa hutoa matamko ya kuzizuia mamlaka mbalimbali zisiwaguse machinga kwa madai kuwa ndiyo wapigakura na watu muhimu kwa vyama vyao.

Twende mbele turudi nyuma hii haikubaliki.

> **Miongoni mwa sababu kubwa zinazochangia mizozo isiyokwisha kati ya halmashauri na wamachinga ni wanasiasa kuwatumia wafanyabiashara hao kama mtaji wao hususan unapokaribia Uchaguzi Mkuu.**

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

rasilimali za Wizara. Shughuli za programu hii ndogo zinatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu hii ilipangiwa jumla ya **TSh. 11,658,958,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 6,251,182,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 5,407,776,00** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 10,537,030,611** sawa na asilimia **90** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 42 hadi 43.

***Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti***

43. ***Mheshimiwa Spika***, Madhumuni makubwa ya Programu hii ni kufanikisha na kuratibu utekelezaji wa Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh. 10,999,859,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 2,963,500,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TSh. 824,319,000** ni kwa ya ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi na **TSh. 7,212,040,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2024 Jumla ya **TSh. 1,698,728,222** sawa na asilimia **15** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii na matokeo ya muda mfupi ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 43 hadi 46

***Programu ndogo ya Uratibu shughuli za Elimu Pemba***

44. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ndogo ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Msimamizi Mkuu wa shughuli za programu hii ni Afisa Mdhamini wa Elimu Pemba. Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **TSh. 3,766,154,277**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 3,416,154,277** ni kwa ajili ya mishahara na **TSh. 350,000,000** ikiwa ni matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 1,867,028,661** sawa na asilimia **50** zimepatikana. Fedha za programu hii zilitumika katika kusimamia na kufuatilia shughuli zote na programu za elimu Pemba.

***MAPATO***

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kukusanya mapato kupitia usajili wa Skuli za binafsi, malipo ya leseni za walimu, ada za usajili wa skuli, ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita na usajili wa wanafunzi wa skuli binafsi wanaofanya mitihani ya Taifa na usajili wa vituo vya kufanyia mitihani. Hadi kufikia Aprili 2024, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekusanya jumla ya **TSh. 263,884,529** kati ya **TSh. 396,396,336** zilizopangwa kukusanywa. Hii ni sawa ya asilimia **67** ya makadirio. Kati ya mapato yaliyokusanywa **TSh. 94,182,676.50** zinatokana na malipo ya leseni za walimu, **TSh. 38,614,932.50** za usajili wa skuli za binafsi, **TSh. 123,396,920** usajili wa wanafunzi wa skuli binafsi wanaofanya mitihani ya Taifa pamoja na usajili wa vituo vya kufanyia mitihani na **TSh. 7,690,000** za makusanyo ya ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita**.**

***MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2024/2025 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU.***

46. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 naomba sasa niwasilishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kuzingatia vipaumbele vya Wizara.

***Vipaumbele vya Wizara***

47. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaendelea kutekeleza mapendekezo ya ripoti ya mageuzi ya sekta ya Elimu kwa kutekeleza vipaumbele 9 vifuatavyo: -

i) Kuimarisha uongozi na usimamizi wa elimu katika ngazi zote za elimu zikiwemo Skuli, Wilaya, Mkoa na Wizara.

ii) Kuimarisha mfumo wa tathmini ya maendeleo ya elimu ya wanafunzi katika ngazi zote za elimu na kupandisha ufaulu wao.

iii) Kuimarisha miundonmbinu ya Elimu kwa kujenga madarasa 1500 kupitia ujenzi wa Skuli za Ghorofa, Skuli za Chini na kukamilisha madarasa yaliyoanzishwa na wananchi kwa Unguja na Pemba, nyumba 20 za walimu, Ofisi ya Wizara, Ofisi 4 za Elimu Wilaya, vyoo 300, Dakhalia 8 zikiwemo dakhalia za wanaume za Chwaka Tumbe na Paje Mtule pamoja na kuzifanyia ukarabati mkubwa na mdogo skuli 100 za Msingi na Sekondari.

iv) Kujenga karakana (workshop) za Elimu ya Amali katika skuli 33 za Sekondari Unguja na Pemba (karakana 3 kwa kila Wilaya) na kujenga uzio katika skuli ya Sekondari ya Hasnuu Makame na Mohamed Juma Pindua.

v) Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kufundishia na kujifunzia kwa kuziunganisha na mkonga wa taifa taasisi za Elimu zikiwemo; skuli 217 za Sekondari, Vituo vya walimu 12 na Vituo vya Ubunifu wa Kisayansi (Hubs) 22 pamoja na kuzipatia vifaa vya TEHAMA.

vi) Kuendelea kutekeleza mtaala mpya wa umahiri kwa elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari kwa kuwapatia walimu mafunzo na vifaa vya kujifunzia na kufundishia vikiwemo vya Watoto wenye mahitaji maalumu.

vii) Kuimarisha Mafunzo ya Ufundi na Amali kwa kujenga vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali, utanuzi wa Chuo cha Karume (KIST) na ujenzi wa chuo cha ubaharia na kuzipatia vifaa.

viii) Kuimarisha Elimu ya Juu kwa kuongeza fursa ya upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kuanzia ngazi ya Diploma; kuanza mradi wa kujenga kampasi ya kudumu ya Chuo cha IIT Madrasa; Ujenzi wa Jengo la Skuli ya kilimo, Jengo la maabara ya sayansi ya kisasa - SUZA, Ujenzi wa skuli ya Afya, skuli ya meno na kliniki yake -SUZA.

ix) Kuimarisha huduma za maktaba kwa kuanza kujenga maktaba mpya ya kisasa Pamoja na kuimarisha maktaba mtandao (e-library).

48. **Mheshimiwa Spika**, Sasa naomba kuwasilisha mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mfumo wa programu kama ifuatavyo: -

49. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendelea kutekeleza malengo yake yaliyozingatia malengo ya Taifa ya Dira 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), Mapendekezo ya ripoti ya mageuzi ya Sekta ya Elimu Zanzibar, Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na mikakati mengine ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma bora ya elimu nchini. Wizara pia, itaendelea kushirikiana na sekta nyengine zinazotoa huduma za jamii na kuimarisha uchumi ikiwemo Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Maji na Nishati, Idara maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha Wizara itaendeleza mashirikiano na washirika wa maendeleo wa ndani na nje na mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi kwa ujumla katika utekelezaji wa mpango wake kupitia programu sita na miradi mbalimbali ya maendeleo ya elimu.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara itatekeleza miradi mitatu ya maendeleo ambayo ni: -

i. Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya elimu

ii. Mradi wa Uimarishaji wa Ubora wa Elimu kupitia Upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, Mafunzo ya Walimu na Matumizi ya TEHAMA

iii. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu.

***MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU***

51. ***Mheshimiwa Spika***, yafuatayo ni maelezo ya programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yanayohusisha Madhumuni, Matokeo ya muda mfupi, Viashiria na Shabaha za utekelezaji kwa kila programu.

***PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI***

52. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mtoto kimwili na kiakili kwa ajili ya kupata elimu ya maandalizi na msingi na kumuwezesha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na kumtayarisha kwa elimu ya Sekondari.

Jumla ya **TSh. 236,293,613,698** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 117,599,363,698** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 118,694,250,000** kwa kazi za maendeleo.

Matarajio ya matokeo ya utekelezaji wa programu hii, viashiria vya matokeo na shabaha iliyowekwa kwa Mwaka 2024/2025 inajionesha kuanzia ukurasa wa 51 hadi 52.

***PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI***

53. ***Mheshimiwa Spika***, Programu ya Elimu ya Sekondari madhumuni yake makubwa ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kuendelea na masomo katika ngazi za juu zaidi. Jumla ya **TSh. 242,537,540,535** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 111,428,040,535** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 131,109,500,000** kwa kazi za maendeleo.

Matarajio ya matokeo ya utekelezaji wa programu hii, viashiria vya kupima matokeo na shabaha iliyowekwa ni kama inavyojionesha kuanzia ukurasa wa 52 hadi 53.

***PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU***

54. ***Mheshimiwa Spika***, programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujiajiri au kuajiriwa**.** Programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni mafunzo ya ualimu na maeneo manne ya huduma, ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti; Huduma ya Sayansi na Teknolojia; Huduma ya

*Inaendelea uk. 8*

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.

Jumla ya **TSh. 210,747,937,698** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 35,981,775,698** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 174,766,162,000** kwa kazi za maendeleo.

Matarajio ya matokeo ya utekelezaji wa programu hii, viashiria vya kupima matokeo na shabaha iliyowekwa ni kama inavyojionesha katika ukurasa wa 54 hadi 59.

***PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI***

55. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa mwanafunzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Programu hii ina programu ndogo mbili; Mafunzo ya Amali yenye lengo la kutoa elimu itakayowawezesha vijana kujiajiri ili kujikwamua na umasikini na Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima yenye dhumuni la kupunguza kiwango cha wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanajamii.

56. Jumla ya **TSh. 41,002,809,755** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 11,502,809,755** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 29,500,000,000** kwa kazi za maendeleo.

Matarajio ya matokeo ya utekelezaji wa programu hii, viashiria vya kupima matokeo na shabaha iliyowekwa ni kama inavyojionesha katika ukurasa wa 59 hadi 61.

***PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU***

57. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu na imejengwa na Programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma.

Jumla ya **TSh. 48,565,662,396** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 14,920,662,396** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 33,645,000,000** kwa kazi za maendeleo. Programu hii ina programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama yafuatayo:-

***Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia***

58. ***Mheshimiwa Spika***, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu.

***Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu***

59. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utekelezaji wa utoaji wa elimu.

***Huduma ya Ukaguzi wa Elimu***

60. ***Mheshimiwa Spika***, utoaji wa huduma hii una madhumuni ya kusimamia utoaji wa elimu unaofuata mtaala na kuhakikisha ufanisi na ubora wa elimu inayotolewa.

***Huduma za Maktaba***

61. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu na vyanzo vyengine vya taaluma kwa wananchi.

***Huduma ya Urajisi wa Elimu***

62. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na taratibu za Wizara zinafuatwa, kutoa leseni kwa walimu na kusajili skuli za Serikali na za binafsi.

***Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha***

63. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu kwa wote wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum, kutoa elimu ya stadi za maisha ikijumuisha ushauri na unasihi, jinsia, nidhamu endelevu, madawa ya kulevya na masuala yanayohusiana na afya ya uzazi.

***Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)***

64. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kuifanya teknolojia ya habari na mawasiliano itumike katika kujifunza, kufundisha, ngazi ya utawala na katika maisha ya kila siku.

***Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni***

65. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo.

Matarajio ya matokeo ya utekelezaji wa programu hii, viashiria vya matokeo na shabaha iliyowekwa kwa mwaka 2024/2025 ni kama inavyojionesha Kuanzia ukurasa wa 61 hadi 67.

***PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI***

66. ***Mheshimiwa Spika***, Programu hii madhumuni yake makubwa ni kuhakikisha nyenzo zilizo bora zinapatikana na zinatumika kwa kuimarisha utoaji wa elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu kama zifuatazo:-

Jumla ya **TSh. 51,808,137,918** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 21,458,137,918** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 30,350,000,000** kwa kazi za maendeleo.

***Programu ndogo ya Uongozi kiujumla***

67. ***Mheshimiwa Spika***, programu hii ndogo ina madhumuni ya kuratibu usimamizi na ufanisi wa Uongozi na Utawala wa rasilimali za Wizara.

***Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti***

68. ***Mheshimiwa Spika***, programu hii ina madhumuni ya kufanikisha na kuratibu Mipango, Sera na Utafiti katika Wizara.

***Programu ndogo ya kuratibu shughuli za Elimu Pemba***

69. ***Mheshimiwa Spika***, programu hii ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Matokeo ya muda mfupi na viashiria vya utekelezaji vinavyotumika ni kama vile vilivyoelezwa katika programu za uongozi kiujumla na uratibu wa shughuli za Mipango, Sera na Utafiti.

Matarajio ya matokeo ya utekelezaji wa programu hii, viashiria vya kupima matokeo na shabaha iliyowekwa kwa mwaka 2024/2025 ni kama inavyojionesha katika ukurasa wa 68 na 69.

***MAKADIRIO YA MAPATO***

70. ***Mheshimiwa Spika***, Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakadiria kukusanya jumla ya **Tsh. 1,140,703,000/-** ikiwa ni mapato kutoka katika vyanzo vyake vikuu ambavyo ni usajili wa Skuli za binafsi, malipo ya leseni za walimu, ada za usajili wa skuli, ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita na ada za usajili wa wanafunzi wa skuli binafsi wanaofanya mitihani ya Taifa pamoja na usajili wa vituo vya kufanyia mitihani.

***JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI***

71. ***Mheshimiwa Spika***, Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Jumla ya **TSh. 830,955,702,000** zitahitajika katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya sekta ya Elimu kwa matumizi ya kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **TSh. 618,400,398,000** ni kutoka SMZ na **TSh. 212,555,304,000** ni kutoka kwa wahisani. Kwa fedha za SMZ, **TSh 308,794,998,000** kwa ajili ya kazi za Maendeleo na **TSh 309,605,400,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida yanayojumuisha **TSh. 213,900,000,000** za Mishahara, **TSh 45,491,700,000** za matumizi mengineyo na **TSh. 50,213,700,000** kwa ajili ya Ruzuku kwa Taasisi za Wizara zinazopokea ruzuku. Aidha, jumla ya **TSh. 212,555,304,000** ni kutoka kwa Wahisani. Kati ya fedha hiyo, **TSh. 3,285,290,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 209,269,914,000** ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo.

***SHUKURANI***

72. ***Mheshimiwa Spika***, nachukuwa fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa washirika wote wa maendeleo ya elimu wa ndani na nje waliotuunga mkono na kutoa mashirikiano katika utekelezaji wa mpango wa sekta ya elimu. Miongoni mwa washirika hao ni wanafunzi wenyewe, wazazi, washirika wa maendeleo na mashirika ya misaada ya kimataifa. Tunatoa shukurani zetu za pekee kwa mashirika mbalimbali yakiwemo, Sida, USAID, UNESCO, UNICEF, GPE, Good Neighbours, KOICA na Table for Two. Pia shukurani zetu za dhati kwa Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Napenda pia, kuyashukuru mashirika yasiyo ya kiserikali yakiwemo Milele Zanzibar Foundation, Madrasa Early Childhood Program Zanzibar, "Mwanamke Initiative Foundation", "Zanzibar Maisha Bora Foundation", Save the Children, Book Aid International, ZAYEDESA, JUWASEZA, ZATU na Mtandao wa Elimu Zanzibar. Vile Vile napenda kuyashukuru makampuni na mashirika mbalimbali ya kifedha yakiwemo Benki ya Watu wa Zanzibar, CRDB, NBC, NMB, Tanzania Postal Bank, Equity Bank, Amana Bank, TigoZANTEL, Airtel, Vodacom, Azam Marine, Zan Fast Ferries na SACCOS mbalimbali kwa misaada yao katika sekta yetu ya elimu na kwa wafanyakazi kwa ujumla. Shukurani za pekee ziende katika Mabaraza ya Miji kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuchangia maendeleo ya elimu Zanzibar.

73. ***Mheshimiwa Spika***, Shukurani za pekee kwa Chama changu cha Mapinduzi kuanzia Taifa hadi Shina kwa kuwajali wananchi wote na kuendelea kusimamia maendeleo kwa taifa letu. Aidha, shukurani kwa familia yangu kwa ushirikiano wanaonipatia.

74. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa viongozi wenzangu kuanzia wewe Mheshimiwa Spika kiongozi wetu, Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa mnaoendelea kunipa na kwa namna mtakavyoichangia hotuba yangu hii, nasema ahsanteni sana.

75. ***Mheshimiwa Spika***, mwisho sio kwa umuhimu, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru familia yangu, ndugu, jamaa na marafiki wote kwa kunivumilia na kunitia moyo katika majukumu yangu.

76. ***Mheshimiwa Spika***, sasa naliomba Baraza lako Tukufu iidhinishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya jumla ya TSh. 830,955,702,000/- kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ili kuiwezesha Wizara yetu hii kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Mei 29 - Juni 4, 2024 |

JAMII

UCHUMI

SIASA

Jarida hili haliuzwi




# Naona dalili za wapinzani wengi kuja CCM 2025

UK. 12 & 13

# Nyuki rafiki wa binadamu kwa afya na uchumi - 1



**Na Dkt. Felician Kilahama**

NAPENDA kuanza makala hii kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliye mwingi wa Rehema na mwenye haki; kwa kunijaalia zawadi ya uhai na afya njema tangu kuzaliwa hadi sasa.

Kipekee napenda kumshukuru pia kwa kuniwezesha kufika katika Jiji la Dodoma salama bila ya kikwazo chochote: Jina lake Mungu wetu lihimidiwe. Vilevile, nichukue fursa hii kushukuru Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Idara ya Misitu na Utalii kwa kunialika na kuniwewezesha kuwa mmoja wa washiriki wakati wa Kuadhimisha siku ya Nyuki Duniani.

Tukio hili muhimu la kihistoria lilifanyika Mei 20, 2024 kwenye Ukumbi wa Jakaya Kikwete, ulioko Barabara iendayo Chuo Kikukuu cha Dodoma (UDOM) na viunga vyake katika Jiji la Dodoma.

Historia inaonesha kuwa Baraza la Umoja wa Mataifa (United Nations) Jijini New York, Marekani; wakati wa Kikao cha Disemba, 2017; lilipitisha Azimio kwamba kila tarehe 20 ya Mwezi Mei kila mwaka, iwe Siku Maalumu kwa mataifa kuadhimisha umunhimu wa Nyuki kwa maisha ya wanadamu na mazingira kwa ujumla.

Uamuzi huo ulienda sambamba na Azimio la Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) la mwaka 2015 ambalo lilikuwa na maudhui hayohayo.

Kwa muktadha huo, Tanzania imekuwa ikiadhimisha siku ya nyuki duniani. Kitaifa adhimisho la mwaka huu Mei 20, 2024 lilifanyika Jijiji Dodoma, na Mgeni Rasimi akiwa Dk. Philip Mpango, Makamu wa Rais, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Adhimisho lilihudhuriwa na wadau wengi kiasi kwamba Ukumbi wa Jakaya Kikwete ulifurika sana; kukawepo na shamrashamra za aina yake kuonyesha umuhimu wa nyuki katika maisha ya binadamu. Kadhalika, Mheshimiwa Angela Kairuki, Waziri mwenye dhamana ya kusimamia sekta ya Misitu na Nyuki, akawa mwenyeji na mhusika mkuu kwenye adhimisho hilo.

Waziri aliambatana na Dastun Kitandula, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Dk. Hassan Abbas, Katibu Mkuu pamoja na Timu nzima ya Menejimenti ya Wiraza.

Vilevile, alikuwepo Dk. Suleiman Saidi Jafo, Waziri wa Nchi, mwenye dhamana ya Sekta ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Wengine waliohudhuria ni pamoja na Kamati ya Bunge inayosimamia shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa niaba ya Bunge, ikiongozwa na Najma Murtaza Giga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Chama cha Mapinduzi (CCM) ambacho ndicho Chama Tawala tangu enzi za chama cha TANU (Tanganyika African National Union) kilipoungana na Chama cha Afro-Shiraz Party (ASP) na kuanzisha CCM mwaka 1977, hadi sasa; kiliwakiliswa na wajumbe wake mahusus wakiongozwa na Donald Mejitii, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Bahi.

Kadhalika, walishiriki wadau mabalimbali ikiwa ni pamoja na: wawakilishi wa dini ambao pia walitoa huduma ya maombi na dua wakiitakia amani na maendeleo endelevu huduma ya kiikolojia itolewayo na nyuki kwa afya na maendeleo yetu pamoja na uhifadhi wa mazingira.

Vilevile, walihudhuria wanawake, vijana, na wasanii, akiwemo mhamasisha wa kutunza mazingira, Msanii mahiri Bwana Mrisho Mpoto Pamoja na baadhi ya wazee na wafugaji nyuki kutoka sehemu mbalimbali nchini, hawakusahaulika.

Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii; pia iliona vyema adhimisho la tano kuhusu siku ya nyuki duniani, liambatane na onyesho la shughuli zinazofanywa na wajasiriamali pamoja na wadau wengine wanaojihusisha na biashara ya mazao ya nyuki. Hivyo, adhimisho kwa mwaka 2024, lilihusisha wajasiriamali/wadau wapatao 90 walioshiriki kikamilifu tangu Mei 17, 2024 wakionesha mazao/bidhaa mbalimbali kutokana na kazi nzuri inayofanywa na 'nyuki' ikiwemo: asali (itokanayo na nyuki wanaouma na wasiouma), nta, chavua (pollen) inayokusanywa na nyuki wakati wa kutafuta malighafi ya kujitengenezea chakula wenyewe na malikia wao. Katika harakati hizo, nyuki huweza kutembelea maua mengi na hivyo kukusanya chavua ya kutosheleza mahitaji yao lakini binadamu, kwa neema na uwezo tunaojaliwa na Mwenyezi Mungu, pia huweza kukusanya sehemu ya chavua waliyoipata kabla hawajaingia kwenye mizinga ili kuweza kutengeneza asali ambayo pia binadamu anaichangamkia inapokuwa tayari.

Kabla ya kuingia kwenye ukumbi, Mgeni Rasimi alitembelea baadhi ya wadau waliokuwa kwenye maonesho. Moja ya wadau aliowatembelea walikuwa wanafunzi wa Shule ya Msingi iliyoko Wilayani Mvomero, mkoani Morogoro. Shule iliwakilishwa na wanafunzi watatu: wa darasa la nne, la sita na la saba. Hawa walitoka kwenye shule ambazo zimejiunga na programmu jumuishi ya Eco-schools inayoendeshwa na shirika la kutunza na kuendeleza misitu nchini yaani: Tanzania Forest Conservation Group (TFCG), lenye makao yake Dar-es Salaam kupiti msaada kutoka Serikali ya Denmark ili kuwezesha utekelezaji.

Wadau wengine waliopata bahati ya kutembelewa na Makamu wa Rais, walikuwa ni Malikale na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS). Wengine wakikuwa wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Kijiji cha Nyuki Co. Ltd kutoka Mkoani Singida. Baadaya ya hapo, Mgeni Rasmi pamoja na alioambatana nao, wakaingia ukumbini ili Siku ya Nyuki Duniani iweze kuadhimishwa kitaifa ipasavyo.

Kwa Tanzania ni madhimisho ya tano tangu Baraza la Umoja wa Mataifa kuiweka bayana Mei 20, kuwa siku maalumu kwa mataifa kuweza kuiadhimisha na kuudhihirisha umuhimu wa viumbe wadogo 'nyuki' katika mustakabali mzima wa maisha yetu wanadamu na jinsi wanavyotusaidia kuyaboresha maisha kupitia mazao mbalimbali yatokanayo na kazi kubwa inayofanywa na nyuki bila kuchoka, wala kukata tamaa kutokana na usumbufu wanaoupata kutoka kwa baadhi yetu wanadamu na wanyama waharibifu.

Kaulimbiu kwa madhimisho ya mwaka huu, ilikuwa ni: **Nyuki kwa Afya na Maendeleo: Tuwatunze**. Kiini cha kaulimbiu hiyo ni kuonyesha jinsi gani nyuki ni rafiki wa binadamu.

Kwa maneno mengine, ni kuwahakikishia Watanzania kuwa uwepo wa viumbe nyuki ni muhimu kwa afya zetu lakini pia kwa maendeleo ya taifa. Kabla ya Mgeni rasmi kutoa hotuba yake, Msanii Bwana Mpoto alishauri, kupitia hamasa yake, kuwa nyuki wasiitwe wadudu nyuki' maana kwa kuwaita hivyo ni kutowatendea haki kutokana na kazi muhimu wanayoifanya kuwezesha binadamu kuimarisha afya na kuboresha mazingira.

Akitoa salaamu zake, Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa, Dodoma alisema: Ufugaji nyuki ni shughuli ya kiuchumi. Mathalani, Tanzania kuna wafugaji nyuki, pamoja na wauzaji mazao ya nyuki, wenye viwanda kuchakata mazao ya nyuki na wasambaji, zaidi ya milioni mbili. Hivyo, nyuki ni rasilimari muhimu kwa kuzingatia kuwa ni chanzo cha ajira kwa watanzania wengi.

Mkuu wa Mkoa, akashauri tutunze mazingira ili kuwawezesha nyuki kuendelea kuwepo kwa wingi kwa faida yetu akamalizia kwa kusema acha shoka tundika mizinga.

Kadhalika, Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii; aliona vyema kusema machache kabla hajafanya utambulisho ili walioshiriki hafla hiyo waweze kuuona umuhimu wa nyuki kwa afya za watu.

Kwanza, alianza kwa kumtaja Hayati 'Mohamed Ali' aliyejulikana kuwa ni mfalme wa mchezo wa ngumi duniani, kuwa wakati wa uhai wake aliwahi kusema elea kama kipepeo na/au dunga kama nyuki *(float like butterfly and/ or 'sting like a bee')*. Kwa usemi huo, alionesha kuwa nyuki siyo wa kuchezewa hovyo maana ni kiumbe hatari kwa wanaomchezea isivyotakiwa; lakini pia usemi huo ukionyesha jinsi huyo mfalme wa ngumi duniani alivyokuwa wa kuogopwa: akidunga ngumi moja tu mpinzania wake anaanguka chini.

Vilevile, Katibu Mkuu aliongeza kuwa hata zamakale, umuhimu wa 'nyuki' kwa uhai wa binadamu ulijulikana. Alifafanua kuwa umuhimu wa nyuki umedhihirishwa ipassavyo kwenye Vitabu vya Dini' zote.

Akitoa mifano michache, Dkt. Abassi alisema katika Biblia Takatifu maelezo kuhusu nyuki yanapatikana kwenye vitabu kama: Kumbukumbu la Torati; Mithali; Isaya na Waamuzi. Alitaja Kitabu cha Waamuzi 14:8-9 kuthibitisha alichokisema. Kadhalika, akasema kwenye 'Quran Tukufu' Sura ya 16 inaeleza habari njema na umuhimu wa nyuki". Baada ya kuyasema hayo akafanya utambulisho wa wadau wote waliohudhuria na kushiriki maadhimisho ya siku ya nyuki duniani. **Itaendelea.**



Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Wekeni bajeti madhubuti za matangazo na muwalipe wanahabari

HEBU jaribu kufumba macho na kufikiria hali itakuwaje kama itapita siku moja kukiwa hakuna taarifa yoyote kupitia vyombo vya habari!

Yaani alfajiri hadi saa sita usiku kukawa hakuna redio yoyote inayosikika, hakuna televisheni, gazeti wala taarifa yoyote kupitia mitandao ya kijamii ya chanzo au chombo chenye kuaminika!

Halafu iwe kwamba siku hiyo, viongozi wengi wanashiriki hafla mbalimbali zinazogusa wananchi na maendeleo kama si kushughulikia kero zao (wananchi).

Kwa mfano siku hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anashiriki mkutano wa kimataifa kuhusu amani jijini Dar es Salaam, Waziri Mkuu anagawa misaada kwa watu walioathirika na mafuriko Lindi, Naibu Waziri Mkuu anazindua Wiki ya Maji Tanga, Waziri wa Ujenzi anakagua barabara iliyokatika Maswa, Waziri wa Afya anapokea msaada wa vifaa tiba kutoka Marekani, kuna nusu fainali ya Kombe la Shirikisho na kadhalika na kadhalika huku Bunge likiendelea na shughuli zake pale Dodoma.

Ninachotaka kusema hapa ni kwamba yote hayo yanakufukia kila siku kwa sababu wanahabari wako kazini. Kuna watu wanawekeza fedha kwa ajili ya kununua vifaa mbalimbali kama kompyuta, simu, kamera, simu, kulipa mishahara, kodi ya jengo na gharama nyingine lukuki za uendeshaji ili habari zikufikie.

Nikirudi pale bungeni Dodoma, sasa hivi tuko katika kipindi cha bajeti ambapo Wizara mbalimbali zinawasilisha makadirio ya mapato na matumizi (bajeti) kwa ajili ya mwaka wa fedha wa 2024/2025.

Katika mawasilisho ya mawaziri utasikia wakisema kiasi kadhaa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi kadhaa ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Matumizi ya kawaida ni mambo kama mishahara, posho na manunuzi mbalimbali. Lakini kwenye shughuli za maendeleo mara nyingi ni pamoja na miradi mbalimbali ambayo wizara inatarajia kufanya kwa ajili ya wananchi na hivyo miradi inatakiwa wananchi kuifahamu na kuwa tayari kuipokea.

Ni kwa mantiki hiyo, ni muhimu kwa wizara na taasisi zake kutangaza shughuli hizo za maendeleo kwenye vyombo vya habari ili wananchi wafahamu na kuwa tayari kutoa ushirikiano.

Je, wizara zinatangaza shughuli hizo kwa uhakika ili kuwafikia walengwa? Zinaweka bajeti kwa ajili hiyo na kama zinaweka bajeti inatumika kama ilivyokusudiwa kwa maana ya kutangaza na kuvilipa vyombo hivyo vya habari kwa wakati.

Kimsingi, waandishi wa habari wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kuwafikishia wananchi taarifa mbalimbali za viongozi wao na zinazohamasisha maendeleo. Vyombo vya habari pia vimekuwa vilifanya kazi kubwa kubwa kunapokuwa matukio muhimu kama tulipofikwa na janga la UVIKO-19 sambamba na kufikisha kwa umma ajenda mbalimbali za serikali.

Hebu fikiria kama vyombo vya habari visingetoa mchango wake muhimu wakati wa janga la UVIKO-19 hali ingekuwaje?

Ni katika muktadha huo, serikali ina dhima ya kutangaza kwa wingi taarifa muhimu kwa wananchi na kuvilipa hivi vyombo.

Lakini, mbali na baadhi ya mawaziri na wakuu wa taasisi na idara za serikali kutojali kufanya matangazo kupitia vyombo vyetu vya habari na kuvilipa, wale wanaoamua kutangaza wamekuwa hawajali kuvilipa vyombo hivi kwa wakati.

Halmashauri za majiji, manispaa mbalimbali, halmashauri za miji na wilaya, huwa zina shughuli nyingi za maendeleo ambazo wananchi hutakiwa kuzifahamu na zimekuwa na utayari mkubwa wa kutangaza shughuli zao ili kufahamika kwa wananchi, takribani muda wote.



**Waziri wa Habari na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye**

Lakini taasisi ambazo zimekuwa na ugumu sana kuvilipa vyombo vya habari unadhani zimerogwa ni hizi halmashauri. Ninakumbuka chombo kimoja cha habari, kiliamua kupiga marufuku kupokea matangazo ya hizi halmashauri kutokana na usugu wa kutolipia matangazo wanayotoa kiasi kwamba wakati mwingine gharama za kufuatilia malipo zinakuwa kubwa kuliko hata malipo yenyewe.

Ni kutokana na tatizo la madeni makubwa ya taasisi za kiserikali, mbunge wa Viti Maalumu, Ester Bulaya hivi karibuni ameikumbusha Serikali kulipa madeni ya vyombo vya habari ili viweze kujiendesha.

Kwa mujibu wa Bulaya, Serikali inadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 18 na vyombo mbalimbali vya habari ambavyo vinategemea matangazo kutoka serikalini.

Mwanzoni mwa mwezi huu wa Mei katika mkutano wa kitaaluma wa habari, Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Dotto Biteko alikaririwa akisema kwamba atamwomba Waziri Mkuu na viongozi wengine wa serikali wazisihi taasisi za umma kuanza kulipa madeni ya matangazo wanayodaiwa na vyombo vya habari.

Hali kadhalika, katika hotuba yake ya Bajeti kwa mwaka 2024/2025 pamoja na mazungumzo yake kwenye majukwaa mbalimbali ikiwemo Siku ya Uhuru wa Habari, Waziri wa Habari na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye naye amekiri pia kwamba hali ya vyombo vya habari nchini si nzuri sana kiuchumi na sababu moja wapo ni taasisi za umma kupunguza kufanya matangazo na vyombo vya habari na/au kutolipa madeni.

Nape pia alikaririwa na vyombo vya habari akishangaa habari za uchunguzi kupungua kwenye vyombo vya habari.

Alisema pia kwamba anatamani kuona wananchi wenye matatizo na kero mbalimbali wakitumia vyombo vya habari kufikisha malalamiko yao kuliko kwenda kwenye vyombo vya dola (polisi) na wanasiasa.

Ikumbukwe kwamba, mwanzoni mwa mwaka jana, Waziri Nape aliunda timu ya watu 10 chini ya uwenyekiti wa mwanahabari nguli nchini, Tido Mhando ili kutathmini hali ya uchumi katika vyombo vya habari nchini.

Mwezi Mei mwaka jana kamati hiyo iliongezewa muda wa miezi sita uliokuwa unaisha Novemba mwaka jana.

Kwa maana hiyo kamati ilishamaliza kazi na kukabidhi ripoti yake lakini mimi sijawahi kusikia mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti ya kamati hiyo. Pengine nimepitwa. Nitazidi kufuatilia.

Kwanza ninapongeza hatua ya serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuunda kamati kufanya tathmini ya uchumi wa vyombo vya habari na kutoa mrejesho ni hatua za kuchukua ili kuvinyanyua.

Natumaini, moja ya mapendekezo ya kamati hiyo litagusia haya ninayojadili hapa kwa maana ya serikali na taasisi zake kutokuwa na bajeti madhubuti za matangazo na pale ziapoweka bajeti, kuichepushia kwenye shughuli nyingine kutokana na kutojali na kuwa sababu ya kutovilipa vyombo vya habari kwa wakati.

Faida ya vyombo vya habari kuwa na uchumi mzuri ni pamoja na hilo alilosema Waziri Nape la kumudu kuandika habari nyingi za uchunguzi kwa kuwa 'stori' za uchunguzi zinahitaji gharama kuzifanikisha na faida ya story hizi inarudi kwa jamii nzima ikiwemo serikali yenyewe.

Na faida nyingine, mbali na kutengeneza ajira na kuziimarisha, ni kujenga maadili zaidi ya wanahabari kama alivyowahi kusema Tido Mhando wakati wa uzinduzi wa kamati yake mwaka jana.

Alisema: "Hali inazidi kwenda mrama na kwa miaka ya hivi karibuni imekuwa mbaya sana kiuchumi, kampuni nyingi za habari zimekuwa katika matatizo makubwa, tumefika mahali waandishi wapo kwenye chombo flani lakini miezi mitatu, minne hadi sita hawajalipwa ila yupo anafanyakazi, hili linafanya waandishi kwenda hata nje ya maadili na misingi halisi ya uandishi wa habari."

Kwa hali yoyote vyombo vya habari vitabakia kuwa mhimili wa nne usiotajwa wazi wa uongozi wa nchi yetu, hivyo ni lazima serikali kuvitumia kwa matangazo ili kufikisha ujumbe kwa wananchi na kuvilipa kwa wakati ili kuvilea. Hili ni jukumu la lazima ingawa haliko kwenye katiba wala sheria.





# Naona dalili za wapinzani wer

Na Hamid Yassin

TANGU kurejea kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa hapa nchini Julai mwaka 1992 na kufanyika kwa uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya mfumo huo mwaka 1995, kumekuwa na wimbi kubwa la wanasiasa kuhama chama kimoja na kujiunga na chama kingine cha siasa na baadhi yao kurudi katika vyama vyao vya awali kulingana na kile kinachoelezwa kuwa ni upepo wa kisiasa.

Kadri miaka ilivyosonga mbele idadi ya vyama vya siasa vyenye usajili rasmi iliendelea kuongezeka huku mwamko wa kisiasa miongoni mwa wanasiasa na wananchi ukishika kasi pia.

Wanachama na wananchi wamekuwa makini katika kufuatilia mienendo ya wanasiasa na sera za vyama vyao. Aidha, mitandao ya kijamii imekuwa na mchango mkubwa sana katika masuala mbalimbali ya kijamii ikiwemo masuala ya kisiasa hapa nchini.

### KUNADI SERA

Tofauti na huko miaka ya nyuma ambapo masuala ya yahusuyo siasa na wanasiasa yalijadiliwa zaidi wakati wa kampeni za uchaguzi ambapo wagombea wa nafasi mbalimbali katika vyama vyao walinadi sera za vyama vyao majukwaani na kutoa nafasi kwa wananchi (wapigakura) kufanya maamuzi kupitia masanduku ya kura siku ya uchaguzi, siku hizi mambo yamebadilika.

Duniani kote vyama vya siasa hushindana kwa sera zinazoelezwa na wagombea wa nafasi za kisiasa ambao nao hupimwa kwa namna ambavyo wanaweza kusimamia utekelezaji wa sera hizo hata katika kipindi ambacho si cha uchaguzi.

Chama kuwa na sera ni kitu kimoja na utekelezaji wa sera hizo ni hatua ya pili ambao ni muhimu sana kwa mustakabali wa taifa na wananchi wake.

### WANASIASA KUCHUNGUZA UPEPO

Katika mfumo wa vyama vingi vya siasa wanasiasa na hasa wale wenye malengo ya kuwania nafasi za uongozi ikiwemo nafasi ya ubunge na urais huchunguza kwa umakini mkubwa upepo wa kisiasa.

Wanapogundua kuwa upepo huo hauko upande wa vyama vyao, huwafanya kufanya maamuzi magumu kuvihama vyama vyao na kujiunga na vyama vingine ambavyo huonekana upepo huvuma na kuelekea upande sahihi wa kushika dola na kuongoza nchi.

Na mara mambo yanapokwenda kombo, baadhi yao huamua kurudi nyumbani ili kuendelea na harakati za kutimiza ndoto zao au kuwa na malengo mengine katika uwanja wa siasa.

Kama inavyotokea katika chaguzi mbalimbali tangu kuingia kwa mfumo huu, katika uchaguzi mkuu uliopita wa mwaka 2020, baadhi ya wanasiasa waliamua kuvihama vyama vyao na kwenda kutafuta nafasi za uongozi kupitia vyama vingine, lengo likiwa ni kutimiza ndoto zao na pengine kuvutiwa na sera za vyama hivyo.

### KAMPENI KABLA YA MUDA

Vyama vingi nchini vimekuwa vikianza kufanya kampeni ya kujitafuta kwenye chaguzi hata kabla ya muda.

Tofauti na vyama vingine na hata katika nchi zingine wanachama wa Chama Cha Mapinduzi hawapaswi kuonesha nia ya kugombea na kuanza harakati hizo kabla ya muda uliowekwa kwa mujibu wa chama chao.


Wanachama na viongozi wanaobainika kuvunja kanuni hizo kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu na wengine kufukuzwa uanachama pale ambapo vikao mbalimbali vya chama vinaporidhia mwanachama huyo kuvuliwa uanachama na zaidi huwa hakuna nafasi ya kukata rufaa.

Makada kadhaa nguli wa Chama Cha Mapinduzi walikumbwa na sekeseke hilo, sina haja ya kutaja majina yao hapa nikiamini wanajulikana. Hawa walituhumiwa kufanya kampeni mapema kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Hata hivyo, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, kati ya hao walikuwepo walioingia katika tano bora za kura za maoni ndani ya chama, lakini hawakufanikiwa kupenya katika tatu bora hivyo ndoto zao za kuukwaa urais kuanza kufifia.

Katika hatua nyingine makada hao wakongwe wa CCM walikabiliwa na makosa mbalimbali ya kimaadili yaliyosababisha kuitwa mbele ya vikao vya juu vya chama ikiwemo Kamati ya Maadili ikiwa ni utaratibu wa chama kuitwa na kupewa nafasi ya kujitetea pale inapotokea malalamiko juu ya





# ngi kuja CCM 2025

mwenendo wa mwanachama.

**KUVULIWA UANACHAMA**

Licha ya mmoja wao kuhojiwa na kupewa nafasi ya kusikilizwa Februari 28, 2020, Chama cha Mapinduzi (CCM) kilimvua uanachama baada ya kutoridhishwa na mienendo yake.

Pamoja na hatua ya kuvuliwa uanachama kada yule hakukata tamaa katika harakati za kutimiza ndoto zake za kisiasa. Badala yake alifanya maamuzi ya kujiunga na chama cha upinzani na baadaye aliteuliwa kupeperusha bendera ya chana hicho kuwania nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Julai, mwaka 2020 alijiunga rasmi na chama hicho cha upinzani na kupewa nafasi ya mshauri wa chama kutokana na uzoefu wake mkubwa katika siasa za ndani na nje ya nchi.

Mbunge huyo wa zamani alionekana kuwa na ushawishi mkubwa wa kisiasa ndani ya chama hicho, hatua iliyopelekea kupewa jukumu zito la kupigania chama hicho kushika dola.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhiwa Ilani ya Uchaguzi Mkuu 2020 ya chama hicho jijini Dar es Salaam, Mgombe urais yule mteule alisema kila mwanachama makini wa CCM anafahamu ukweli uliomo ndani ya chama hicho kikongwe barani Afrika.

"Hata nyinyi mnafahamu kwamba ndani ya chama hicho kuna CCM wapya na kuna wana CCM waliotumbuliwa na kukatwa walipotaka kuja huku nilipo wakakatazwa," alidai mwanasiasa yule.

Alisema kabla ya kujiunga na chama hicho cha upinzani alikuwa akiwasiliana na kiongozi mkuu wa chama hicho tangu Februari mwaka huo wa 2020 wakibadilishana mawazo na kutafuta namna sahihi ya kumkomboa Mtanzania.

**ILANI BORA?**

Alisema hata Ilani ya chama hicho aliyokabidhiwa alichangia mambo kadhaa hasa katika sekta anayoifahamu vyema ya diplomasia ya Kimataifa.

"Ni Ilani bora kuliko zote. Nimekuwa kwenye siasa kwa miaka 38 sasa, nimesoma Ilani za vyama vyote. Lakini hii inatekelezeka na itamkomboa Mtanzania," alieleza huku akishangiliwa na wafuasi wa chama hicho.

Katika matokeo ya Uchaguzi Mkuu mwaka huo alipata jumla ya kura 81,129 sawa na asilimia 0.55 akitimuliwa vumbi vibaya sana na mgombea wa CCM, John Pombe Magufuli aliyepata jumla ya kura 12,516,252 sawa na asilimia 84.40 akifuatiwa na mgombea kwa tiketi ya Chadema Tundu Antipas Lissu aliyepata kura 1,933,271 sawa na asilimia 13.04.

Safari ya mwanasiasa yule ndani ya chama kile ilikamilika Januari mwaka 2021 alipotangaza kujitoa kwenye chama hicho bila kuweka wazi chama ambacho alitarajia kujiunga nacho.

**KUMUUNGA MKONO SAMIA**

Jumanne ya Oktoba 5 mwaka 2021, akiwa mkoani kwao alisema anamuunga mkono Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na alikuwa tayari kumpigia kampeni katika uchaguzi mkuu 2025.

"Niwaombe tusahau yaliyopita tuanze upya tujenge Taifa letu niko tayari kuwa kampeni meneja wa Rais katika Uchaguzi mkuu wa mwaka 2025," alisema Mwanasiasa yule.

Katika ziara ile ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa mwanasiasa yule alisema wakati wowote atakuwa tayari yeye na wananchi wa jimboni mwake kumpa ushirikiano Rais Dk. Samia na serikali yake kwa kuwa ameonesha dhamira ya kuirudisha nchi kwenye misingi ya umoja, mshikamano na uhusiano wa Kitaifa na Kimataifa.

Dk. Samia aliapishwa kuwa Rais wa Sita wa Tanzania Machi 19 mwaka 2021 kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri inayosema; "Endapo kiti cha Rais kitakuwa wazi kutokana na Rais kufariki dunia, kujiuzulu kupoteza sifa za uongozi au kutomudu kazi zake kutokana na maradhi ya mwili na kushindwa kutekeleza kazi na shughuli za Rais basi Makamu wa Rais ataapishwa na atakuwa Rais kwa muda uliobaki katika kipindi cha miaka mitano na kwa masharti yalioelezwa katika Ibara ya 40 ya katiba."

Rais Samia alichukua nafasi ya mtangulizi wake hayati Dk. John Pombe Magufuli aliyefariki dunia Machi 17 mwaka huo 2021 kutokana na maradhi ya moyo.

Kumekuwa na shinikizo la wadau mbalimbali juu kumtaka na kumsihi akubali kugombea nafasi hiyo ya juu katika Uchaguzi Mkuu wa mwakani 2025, hatua ambayo ilimfanya Rais Samia kutoa msimamo wake juu ya gumzo hilo.

**RAIS KUTOKA SANDUKU LA KURA**

Jumatano ya Septemba 15 mwaka 2021 jijini Dar es Salaam Rais Dk. Samia alisema hadi sasa bado Tanzania haijafanikiwa kumpata Rais mwanamke anayetokana na uchaguzi mkuu kwa kuwa aliyepo madarakani amepatikana kwa kudura za Mungu na takwa la katiba, mbali na kauli hiyo alitoa wito kwa wanawake na Watanzania kusukuma ajenda ya kumsaka Rais mwanamke atakayetokana na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

"Rais mwanamke tutamweka mwaka 2025, wanawake oyee," alisema Rais Samia na kuibua shangwe kwa wanawake waliofurika katika ukumbi wa Diamond Jubilee.

"Ndugu zangu mwaka 2025 tukifanya vizuri tutaweka Rais mwanamke na tutakutana hapa tufurahi. Wameanza kutuchokoza kuandika kwenye vigazeti kwamba Samia hana nia, nani kawaambia? Fadhila za Mungu mkononi zikija usiziachie," alisema Rais Dk. Samia.

Mbali na Mwanasiasa niliyemzungumzia kwenye makala haya, pia aliyekuwa Waziri Mkuu katika Awamu ya Nne, marehemu Edward Lowassa aliondoka CCM na kujiunga na Chadema Julai 28 mwaka 2015 na baadaye kugombea Urais kwa tiketi ya chama hicho.

Lowassa ambaye alipata ushindi wa kura 6,072,848 sawa na asilimia 39.7 alirejea tena CCM Machi, Mosi mwaka 2019 na kusema amerudi nyumbani.

Machi, 10 akiwa Monduli marehemu Lowassa alisema alirudi nyumbani na asiulizwe alirudi kufanya nini huku akiwashukuru Chadema kwa mapokezi yao na ushirikiano waliompa wakati wote akiwa huko.

Kuhusu uongozi wa Rais Dk. Samia Mheshimiwa Lowassa alisema.

"Rais Samia amethibitisha pasipo na shaka kwamba Tanzania imepata nyota ya jaha kwa kuwa na kiongozi mkuu mwanamke hodari na shupavu ambaye leo hii tuna kila sababu ya kujivunia na kumuunga mkono."

Mwaka 2015 wanachama na viongozi wengi wa Chama Cha Mapinduzi walihamia vyama vya upinzani na miaka mitatu baadaye wanachama hao na wale wa upinzani walianza kurejea CCM huku wakieleza kuvutiwa na utendaji kazi wa viongozi wa juu wa wakati huo, Dk. Magufuli na Dk. Samia aliyekuwa Makamu wake.

Rais Samia alikuja na kauli mbiu inayosema " kazi Iendelee." Wengi wanaikubali na kuiunga mkono kwa vitendo na hadi sasa sioni dalali ya Wana-CCM kukikacha chama chao kwenda kusaka nafasi za uongozi kupitia vyama vya upinzani. Badala yake naona dalili ya wapinzani wengi kuja CCM.

Naziona dalili hizo kwa sababu ya mambo makubwa ambayo ameyafanya Samia katika kipindi kifupi na kuwa kwenye myoyo ya Watanzania wengi huku sera za CCM zikitekelezwa vyema.

Upande wa upinzani, wameshindwa hata kutumia kipindi hiki kueleza vyema sera mbadala walizo nazo kuzipita zile za CCM.

Badala yake wanaendelea kusubiri makosa ya kibinidamu yafanywe na viongozi wa CCM ili wapate cha kusema na hivi karibuni walianza kuegemea kwenye ukabila wakihoji Uzanzibari wa Rais Samia wakidhani hiyo inaweza kuwasaidia kuungwa mkono na wanchi wa Tanzania Bara (Tanganyika).

***Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.***



# Hedhi salama ni muhimu kwa ustawi na maendeleo

**Na Hamisi Kibari**

ENZI zetu tulikuwa tunaanza darasa la kwanza tukiwa wakubwa kidogo. Mwenye umri mdogo alikuwa na miaka saba lakini wengine walikuwa na miaka minane, tisa, 10 na hata wenye umri wa miaka 11 walikuwepo!

Ni kutokana na hali hiyo, ilikuwa ni kawaida kuona wavulana wengi wakibalehe wakiwa bado shule ya msingi na wasichana lukuki pia wakivunja ungo wakiwa bado katika kiwango hicho cha elimu.

Wasichana ninaowasikitikia hadi leo ni wale waliopata bahati mbaya ya kufikwa na tukio la kuvunja ungo ghafla wakiwa darasani. Hawa walitaniwa sana na vijana kiume eti wamechinja kuku juu ya dawati!

Na kwa kutojua namna ya kukadiria tarehe au kujua dalili, wengine pia walijikuta wakipatwa na hedhi ghafla wakiwa darasani na kuwa mtihani mkubwa kwao.

Kuna wengine waliacha kabisa shule kutokana na hali hiyo wakiona ni fedheha kubwa kwao huku wengine wakiathirika kisaikolojia hadi kushindwa kufanya vizuri darasani.

Haya yote yalitokea kutokana na wazazi na walimu kushindwa kutoa elimu ya hedhi kwa wanafunzi; kwa maana ya wasichana na wavulana kadhalika ili kuliona jambo hilo la kawaida. Pia miundombinu ya vyoo haikuwa rafiki sana, maji yakiwa ya shida huku upatikanaji wa taulo za usafi ukiwa mtihani mkubwa.

Mimi huita kipindi cha ujima cha kuona masuala ya kufundishana haki ya uzazi na ujinsia kama mwiko. Kipindi ambacho mama aliona hana haja kumfundisha binti yake jinsi atakavyokuwa anapata mabadiliko ya kibaiolojia kadri anavyokua, hivyo mtoto kuokotaokota huku na kule kwa watu mbalimbali hadi kwa wahuni.

Ilikuwa ni kipindi ambacho, kila nikiangalia nyuma ninagundua kwamba wasichana niliosoma nao, hasa shule ya msingi mwisho wa miaka 1970 na mwanzoni mwa 1980 walikuwa wanapata shida sana wanapoingia kwenye hedhi na ndio maana wasichana walikuwa wakiongoza kwa kuandikwa utoro kwa sababu wakiwa katika hali hiyo ilikuwa ni vigumu kuja shuleni kwa sababu nyingi; taulo za usafi ulikuwa msamiati, wengi wakitumia vipande vya khanga za mama zao, lakini tabu ilikuwa matundu ya kutosha ya vyoo pamoja na tatizo la upatikanaji wa maji.

Tofauti na siku hizi, enzi zetu wasichana wengi walikuwa wanafeli darasa la saba kulinganisha na sisi wavulana.

Ninakumbuka vyoo vya Shule ya Msingi Musoma niliyosoma mimi ambavyo vilikuwa vyoo vya maji, kuna siku ukiingia unakutana na kinyesi mlangoni na mtu kachambia karatasi au jani la mgomba kutokana na kukosekana kwa maji na ukiingia huko ndani ndio balaa! Yaani wakati mwingine, kwa hali utakayoikuta vyooni, haja, iwe kubwa au ndogo inakata yenyewe! Unalazimika kujikaza 'kisabuni' ukajisaidie nyumbani baada ya muda wa shule.

Kwa kuwa shule ilikuwa karibu na makaburi, wakati mwingine hali ikiwa ngumu unalazimika kwenda huko kama hakuna 'jambo' linaloendelea huko huku pia ukiombea usikutane na mwalimu aliyekwenda huko akiwa na shida kama zako!

Hata hivyo, waliokuwa na ubavu wa kwenda huko ni wavulana lakini sasa ndio nagundua ilikuwa ni dhambi kubwa kujisaidia kwenye makazi ya wafu. Waswahili walisema kweli, shida haina adabu!

Hayo nimepiga 'mastori' ya zamani lakini nimeshangaa kugundua kwamba hata katika zama hizi bado wasichana walio katika baadhi ya shule, bila shaka na baadhi ya vyuo bado wanahangaishwa na mazingira yasiyo rafiki wanapoingia kwenye hedhi.

Ni katika muktadha huo, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu amekaririwa hivi karibuni akiitaka jamii na wadau kuweka mazingira rafiki kwenye suala la hedhi salama ili msichana na mwanamke aweze kutimiza majukumu yake bila kikwazo.

Waziri Ummy alitoa wito huo Mei 22, 2024 Jijini Dodoma wakati akitoa Tamko kwa Umma kuhusu Maadhimisho ya Wiki ya Hedhi Salama na uzinduzi wa maadhimisho ya wiki ya Hedhi Salama.

"Bila Hedhi salama hakuna ustawi, kwa nini tuone kinyaaa kuzungumza masuala ya hedhi salama?" Amehoji Waziri Ummy na kufafanua kwa suala la hedhi salama hatuwezi kulikwepa kwani ni sehemu ya kuendeleza kizazi katika jamii na taifa kwa ujumla.

Hedhi salama ni nini? Waziri anafafanua kwamba maana yake ni mhusika kupata elimu bila kikwazo, huduma katika mazingira ya vyoo, uwepo wa usiri, uwepo maji, vifaa salama na utupaji salama wa vifaa vilivyotumika.

*Inaendelea uk. 18*

# Kazi pevu za Dk. Samia zinavyowaumbua wanafiki

Na Hamid Yassin

MACHI 19 mwaka huu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alitimiza miaka mitatu madarakani tangu aapishwe kuongoza taifa hili la Tanzania ikiwa ni Awamu ya Sita tangu tupate uhuru toka kwa wakoloni wa Kiingereza.

Ni miaka mitatu ya kazi hasa, kama ilivyo kauli mbiu yake aliyoingia nayo madarakani ya 'Kazi iendelee'.



**MIRADI MIKUBWA**

Rais ameendeleza yale yote mazuri ya awamu ya tano ambayo yeye alikuwa Makamu wa Rais na alishiriki kikamilifu kuyaanzisha na kuyasimamia.

Katika miradi yote mikubwa ya kimkakati ameendelea kuidhinisha fedha ili iendelee kama ilivyopangwa. Hii ni kama vile ile ya Reli ya Mwendokasi (SGR), Bwawa la Mwalimu Nyerere, barabara kubwa na ndogo na hata ule mradi wa umeme vijijini (REA) na pia tumeshuhudia ndege zilizonunuliwa zikiendelea kuwasili nchini ndani ya hii miaka mitatu.

**KUFUFUA UCHUMI**

Lakini kama hiyo haitoshi, Dkt. Samia amekuja na mipango yake mingine thabiti ya kufufua uchumi uliyoyumba kwa sababu mbalimbali kubwa ikiwa mtikisiko wa ugonjwa hatari la Uviko 19.

Ameelekeza ukusanyaji mzuri wa mapato ya serikali kutoka kwenye vyanzo mbalimbali hususani kwa wafanyabiashara ambapo ameagiza ule 'ubabe' dhidi yao ukome.

Rais Samia kwa kasi kubwa anarudisha uhusiano ulioteteraka na mataifa mbalimbali na hivi niandikapo makala haya Mama ameshatembelea mataifa kadhaa makubwa na madogo ya nje, ameshahudhuria mikutano mbalimbali ya kimataifa ambayo imekuwa na matokeo mazuri mintarafu suala zima la kuvuta mitaji kutoka nje (uwekezaji) na upatikanaji wa masoko kwa bidhaa za Tanzania nje ya nchi ikiwemo nyama ya mbuzi.

**KERO ZA WANANCHI**

Katika kipindi hiki kifupi pia Rais Samia ameonesha kwamba yeye ni msikivu. Amesikiliza vilio na malalamiko kadhaa ya wananchi anawaongoza na kuyatolea majawabu ya haraka na yenye manufaa kwa raia wake.

Hii ni kama vile tozo za miamala ya simu zilizokuwa zinapaa kila kukicha, ambapo baada ya malalamiko toka kwa wananchi haraka aliviagiza vyombo husika kuliangalia hilo na tayari tozo hizo zimepunguzwa kwa asilimia thelathini na hivi sasa mambo ni shwari.

Amekuwa akitembea kukagua miradi mbalimbali na kuwa mkali kwa ile inayosuasua ambapo sasa tumeshuhudia miradi kadhaa ikienda kwa kasi ya 'kimbunga'.

Huwezi kuyataja yote bila kugusia lile jambo la kuunda Kamati Maalumu ya Ugonjwa wa Uviko 19 chini ya Mwenyekiti wake, Prof. Said Aboud ambapo ilikuja na majibu mazuri ya kumshauri Rais akubali kuidhinisha chanjo ya hiari kwa ugonjwa huo ambapo hivi niandikapo makala haya tayari Watanzania kadhaa wameshachanjwa na wengine wakiendelea kujitokeza kupata chanjo bure, yaani bila malipo yoyote yale.

**Kiu ya Mama Samia kujiendeleza kielimu haijawahi kufikia ukomo kwani mwaka 2015 alihitimu shahada ya uzamili katika Maendeleo ya Uchumi ya Jamii katika programu ya ushirikiano kati ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo kikuu cha Southern New Hampshire cha nchini Uingereza.**

**RAIS SAMIA AMETOKEA WAPI?**

Bi Samia alizaliwa Januari 27, 1960 visiwani Zanzibar ambapo alipata elimu ya msingi kati ya mwaka 1966 na 1972 katika shule tofauti tofauti katika visiwa viwili vikubwa vinavyounda Zanzibar.

Rais Samia alianza safari yake ya elimu katika Shule ya Msingi Chawaka iliyopo kisiwani Unguja na baadaye alihamia Shule ya Msingi Ziwani iliyopo kisiwani Pemba kabla ya kurejea Unguja na kumaliza elimu ya msingi katika Shule ya Msingi ya Mahonda.

Elimu ya Upili ama Sekondari aliisoma kati ya mwaka mwaka 1973 mpaka mwaka 1976 ambapo kama ilivyokuwa kwenye elimu ya msingi, Samia Suluhu Hassan alisoma shule mbili tofauti ambapo alisoma kidato cha kwanza mpaka cha nne katika shule ya sekondari ya Ng'ambo iliyopo Unguja kati ya mwaka 1973-1975 kabla ya kuhamia Sekondari ya Lumumba, iliyopo kisiwani Unguja mnamo mwaka 1976 ambapo alihitimu kidato cha nne.

Baada ya kumaliza elimu ya Sekondari, Dk. Samia hakujiunga moja kwa moja na masomo ya Chuo, kwani mwaka 1977 aliajiriwa kama mchapishaji katika serikali ya Zanzibar ambapo alipanda mpaka ngazi ya kuwa Afisa wa Mipango serikalini kati ya 1987 na 1988.

Wakati akiwa mtumishi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Samia alikuwa akijiendeleza kielimu ambapo alisoma kozi fupi mbalimbali ikiwemo ya cheti cha takwimu kabla ya kujiunga na Taasisi ya Maendeleo na Uongozi ya Mzumbe Morogoro ambapo alihitimu stashahada ya juu ya Utawala mnamo mwaka 1986.

Kati ya mwaka 1992 mpaka 1994 Rais Samia alisoma stashahada ya Uzamili ya Uchumi katika Chuo Kikuu cha Manchester kilichopo nchini Uingereza.

Kiu ya Mama Samia kujiendeleza kielimu haijawahi kufikia ukomo kwani mwaka 2015 alihitimu shahada ya uzamili katika Maendeleo ya Uchumi ya Jamii katika programu ya ushirikiano kati ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo kikuu cha Southern New Hampshire cha nchini Uingereza.

Rais Dk. Samia aliolewa miaka miwili tu baada ya kuhitimu elimu yake ya sekondari kule visiwani Zanzibar mnamo mwaka wa 1978, ambapo alifunga pingu za maisha Bw. Hafidh Ameir, ambaye wakati huo alikuwa Afisa wa Kilimo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo wawili hao wamejaliwa watoto wanne; mmoja kati ya wanawe Bi. Wanu Hafidh Ameir aliyezaliwa mwaka 1982 ndiye anayefuata nyayo za mama yake kwani ni Mwakilishi Maalum katika Bunge la Zanzibar.

Rais Samia mbali na kuhudumu Serikalini tangu amalize masomo yake ya sekondari akiwa na miaka 16, alipata kufanya kazi na mashirika ya kimataifa ambapo kati ya mwaka 1992 mpaka mwaka 1994 alifanya kazi na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula ambapo alihudumu kwa nafasi ya Afisa Miradi.

*Inaendelea uk. 18*



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Mazingira wezeshi ya kuwainua wanawake kiuchumi ni muhimu



Uwezeshaji wanawake kiuchumi ni moja ya mikakati ya serikali yetu. Ni mkakati unaolenga kuwapa fursa za kumiliki mali na kuchangia maendeleo ya familia, jamii na taifa kwa ujumla. Kutokana na umuhimu wa wanawake katika jamii, hakuna namna ambayo familia, jamii na taifa linaweza kusonga mbele kimaendeleo kama kundi hili muhimu la wanawake litabaki nyuma bila kuweka mikakati thabiti ya kuwawezesha hasa katika nyanja ya kiuchumi ambayo kwa miaka mingi wanawake wamekuwa nyuma.

Tukumbuke usemi kwamba ukimwelimisha mwanaume, umeelimisha mtu mmoja lakini ukielimisha mwanamke umeelimisha jamii. Vivyo hivyo naamini ukimwezesha kiuchumi mwanamke, umewezesha jamii kubwa wakati kwa mwanaume unawezesha mtu mmoja.

Mtazamo wa kumwona mwanamke kama mtu wa kubaki nyumbani kulea familia tu bila kujishughulisha katika shughuli za uzalishaji mali unapaswa kubadilika kwani dunia imebadilika sana. Wanawake wamedhihiridha wana uwezo mkubwa wa kumudu majukumu ya uzalishaji mali na hatimaye kuchangia katika maendeleo ya familia na taifa.

Kwa kutambua umuhimu wa wanawake katika ujenzi wa taifa, Mbunge wa Tanga Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ambaye pia ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu wakati wa kujinadi kwenye kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, aliahidi kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili kuwainua wanawake kiuchumi na hatimaye kuharakisha gurudumu la maendeleo.

Ummy Mwalimu ameonesha na anaendelea kuonesha kwamba anatambua uwezeshaji wanawake kiuchumi una mchango mkubwa katika kupunguza umaskini na kuharakisha maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Moja ya mkakati ambao Mbunge huyu wa Tanga Mjini ameusimamia kikamilifu katika kuwainua wanawake ni uundwaji wa jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi wilaya ya Tanga. Uundaji wa jukwaa hili umekuwa na mafanikio makubwa kwani katika kata zote 27 za Jiji la Tanga, kumeundwa majukwaa haya, hii ina maana kuwa kila kata ina jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi.

Uwepo wa majukwaa haya kwenye kila kata unarahisisha ufikiwaji wa wanawake kule walipo na hivyo kuwawezesha kwa kuwapa semina na mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kushiriki shughuli za kiuchumi wakiwa katika vikundi vyao na pia kutoa mikopo itakayowasaidia kuanzisha shughuli za kiuchumi.

Kuwatambua wanawake kule walipo na kupata taarifa zao ni muhimu katika kuhakikisha kuwa mikopo na mafunzo yanayotolewa yanawafikia walengwa husika na hivyo kuepuka uwepo wa vikundi hewa ambavyo ni hatari katika juhudi za kuwainua wanawake kiuchumi.

Ummy Mwalimu amejipambanua kuwa mlezi wa jukwaa la uwezeshaji wanawake Jiji la Tanga. Katika mkutano huo, Ummy amewawahakikishia kushiriki kwenye vikao vyao vya mara kwa mara, kusikiliza changamoto zao na kuzitafutia ufumbuzi ili juhudi za kuwainua wanawake kiuchumi katika Jiji la Tanga ziweze kufanikiwa kikamilifu.

Mei 17, 2024, Ummy Mwalimu alizindua rasmi Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Jiji la Tanga, hafla iliyofanyika katika ofisi za Halmashauri ya jiji la hilo. Katika uzinduzi huo, Ummy amelitaka jukwaa hilo kuwalea na kuwasimamia vizuri wanawake wote katika ngazi za mitaa, kata na tarafa ili kwa pamoja waweze kuinuka kiuchumi.

"Na kwa upande wa jukwaa, nadhani Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Dada Aziza na Katibu wanajua kwenye shughuli za jukwaa nimekuwa nikishiriki na kila mwaka Siku ya Wanawake Duniani nimekuwa nikishiriki kwa kuwa nipo pamoja na jukwaa. Mwenyekiti na timu yako sitawaacha, nitaendelea kufanya kazi na nyie kwa karibu sana kuhakikisha tunajiinua kiuchumi," anasema Ummy Mwalimu.

Uwepo wa jukwaa hili ni muhimu katika kuwaunganisha wanawake pamoja kwa kuwapa mafunzo na mitaji ya kuwawezesha kuanzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi zitakazowasaidia kukuza uchumi na kuchangia maendeleo ya taifa. Ummy anaona umuhimu wa kuwawezesha wanawake kiuchumi na ndiyo maana amemfananisha mwanamke na shingo katika mwili wa binadamu. "Kwa kweli tunasema baba ndiyo kichwa cha familia basi mwanamke ndiyo shingo, bila shingo kichwa hakiwezi kuwepo."

Hii ina maana kuwa juhudi za baba peke yake katika kuinua uchumi wa familia haziwezi kuzaa matunda makubwa kama mama hatajishughulisha, lakini kwa pamoja (baba na mama) wakiunganisha nguvu, familia itasonga mbele kiuchumi kwa kasi kubwa. Na ikumbiukwe kwamba katika zama tulizo nazo tuna akina baba wanaotelekeza familia, wababa walevi na wasiojali mustakabali wa watoto wao na mfano wa hao.

Hali kadhalika kuna akina mama wajane na waliozalishwa kisha wahusika (wanaume) wakakana mimba au kukimbia majukumu. Wanawake hawa wote wanaotakiwa kuwezeshwa, si katika suala la mitaji pekee bali pia elimu ya uzalishaji mali, elimu ya biashara za kisasa ikiwemo matumizi ya intaneti na siku hizi akili mnemba, utendaji wa huduma za taasisi za fedha, utunzaji wa mahesabu hadi utafutaji wa masoko.

Ummy amewapongeza wanawake wa Tanga Mjini kwa jinsi wanavyojituma katika kujiongezea kipato ili kuboresha maisha yao na ya familia zao. Vilevile, amewasisitiza wanawake kutokata tamaa katika kujinyanyua kiuchumi na kujiunga kwenye vikundi rasmi vinavyotambulika ili kuweza kufikiwa kwa urahisi kupitia mikopo nafuu inayotolewa na Halmashauri ya Jiji la Tanga.

**Na kwa upande wa jukwaa, nadhani Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Dada Aziza na Katibu wanajua kwenye shughuli za jukwaa nimekuwa nikishiriki na kila mwaka Siku ya Wanawake Duniani nimekuwa nikishiri kwa kuwa nipo pamoja na jukwaa. Mwenyekiti na timu yako sitawaacha, nitaendelea kufanya kazi na nyie kwa karibu sana kuhakikisha tunajiinua kiuchumi.**

Mimi pia ninachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Ummy kwa kuwashika mkono wanawake hawa na kumhimiza asirudi nyuma katika kutoa mchango wake kuwanyanyua kiuchumi wanawake wa Tanga. Katika uzinduzi huo, Mstahiki Meya wa Jiji la Tanga Abdulrahman Shiloow amesema serikali ina nia thabiti ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, kielimu na katika nyanja zote na ndiyo maana Jiji la Tanga lina majukwaa 27, ukiwa na maana kwamba kila kata ina jukwaa lake la kuwawezesha wanawake kiuchumi.

Kwamba kila jukwaa katika kata linawajibika kupata elimu ya kutosha ili kuwajengea uwezo wanawake wa kata husika katika uchumi, elimu, afya na mazingira. Mstahiki Meya huyo wa Jiji la Tanga amesisitiza kuwa kipaumbele cha kwanza katika majukwaa hayo ni kujengewa uwezo wanawake kielimu na kujitambua, baadaye utoaji wa mikopo unafuata. Hii imekaa vizuri sana.

Aidha, Mkurugenzi wa Jiji la Tanga Dkt. Frederick Sagamiko amemhakikishia Mbunge Ummy Mwalimu kuwa ushiriki wa wanawake wa Jiji la Tanga katika shughuli za kiuchumi ni mkubwa sana na wanapaswa kupongezwa. Mkurugenzi huyo amesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameruhusu kuanzia Julai 1, 2024, mikopo ya asilimia kumi inayotolewa na halmashauri ianze kutolewa, na Jiji la Tanga limetenga zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kuwawezesha wanawake kiuchumi.

Ni wakati mwafaka kwa wanawake wa Jiji la Tanga kuyatumia vyema majukwaa hayo ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ili waweze kuinua vipato vyao kwa maendeleo. Ni vyema hatua kama ya Tanga ikasambaa nchi nzima. Kwamba mikoa mingine isione haya kwenda kujifunza Jiji la Tanga na kuanzisha majukwaa ya kuwawezesha wanawake katika kila kata kwenye maeneo yao.

Mara zote wanawake wakumbuke kuwa wao ndiyo shingo katika mwili wa uchumi, wakibaki nyuma, kichwa peke yake yaani baba atashindwa kufikia maendeleo ya kweli ya familia, hivyo basi, ni muhimu sana wanawake kusimama katika nafasi zao kwa kushiriki katika shughuli za kiuchumi kwa maendeleo endelevu ya familia, jamii na taifa. Mwanamke tafakari, chukua hatua leo.

*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

# Elimu kuhusu Bima - 02

WIKI iliyopita tulianza somo hili lenye makusudi ya kutoa uelewa wa kawaida kwa watu wote kuhusu masuala ya Bima na umuhimu wake. Mambo haya unaweza kuyachukulia kirahisi au kutoyapa uzito sababu hujapatwa na majanga. Lakini kama unataka kuanza kusimama, kama unawaza mbali na kama una malengo makubwa kimaisha ni vyema uwe unaanza kutambua na kujua kuwa kuna maarifa haya muhimu.

Karibu tuendelee na safu hii sehemu ya pili ambapo tunaendelea na aina mbalimbali za mikataba ya bima kwa faida yako na ustawi wetu na wa jamii yetu. Karibu leo tuanzie aina ya tano na kuendelea: -

**(v) Bima mseto (bima kubwa).**

Hii ni bima inayokinga majanga yote ikiwa ni pamoja na majanga ya mtu wa tatu na mwenye chombo cha moto kufidiwa endapo itatokea ajali, chombo kuibiwa au kuungua moto. Ni vizuri kwa mnufaika kuelewa aina ya bima anayonunua na kujua nafasi yake kuhusu chombo chake pale ambapo majanga yatakapotokea.

**(vi) Bima ya moto.**

Hii ni bima ambayo hukinga majengo mbalimbali kama vile nyumba za biashara na za kuishi pale ambapo moto umetokea na kuunguza nyumba. Mmiliki wa Bima hufidiwa kadri ya kima cha bima na masharti yaliyo kwenye mkataba.

Wakati mwingine mtu hukatia bima nyumba bila kuweka bima ya vifaa au vitu mbalimbali vya thamani vilivyo ndani ya nyumba hivyo ni vizuri kutambua aina ya bima unayochukua kulingana na mahitaji.

**(vii) Bima ya dhima**

Ni bima inayotoa kinga dhidi ya madai ya mtu wa tatu kutokana na kuharibiwa mali zake kunakosababishwa na shughuli zako au mali zako unazomiliki. Mfano nyumba yako ikidondoka na kusababisha uharibifu wa nyumba nyingine au hata kifo au maumivu kwa mpita njia sheria inakulazimu kulipa lakini ukiwa na bima ya dhima, kampuni ya bima italipa kwa niaba yako.



(viii) Bima ya ajali

Hii ni bima ambayo inakinga majanga ya ajali ikiwa ni pamoja na maumivu na ulemavu wa muda au kudumu unaoweza kumfanya mtu asiendelee na shughuli zilizokuwa zinampatia mahitaji yake ya kila siku. Bima hii italipa fidia kulingana na viwango vya bima vilivyowekwa kwenye mkataba wa bima husika.

**(ix) Bima ya safari**

Hii hukinga majanga mbalimbali kama ugonjwa, maumivu, kukosa usafiri wa ndege bila kukusudia, kupoteza mzigo katika ndege pia hata kifo kinapotokea bima huwezesha maiti kurudishwa katika nchi ambayo mmiliki wa bima anakotokea kwa ajili ya maziko. Aidha, bima hii hutumika pale ambapo bima za aina nyingine hazitumiki.

**JINSI YA KUPATA BIMA DHIDI YA MAJANGA**

Taratibu ambazo mtu anatakiwa kufuata ili apate bima ni kama ifuatavyo: -

(i) Kabla hujanunua bima pima viwango vya majanga na chagua aina ya bima ambayo inakuwa bora kulingana na majanga yaliyopo;

(ii) Tumia dalali, wakala au kampuni ya Bima iliyosajiliwa na kusimamiwa na TIRA na jadili kwa kina juu ya mahitaji yako ya bima;

(iii) Toa taarifa sahihi kwa dalali, wakala au kampuni ya Bima ili endapo janga linaweza kutokea iwe rahisi kusaidiwa;

(iv) Fanya uchaguzi sahihi wa aina ya mkataba wa bima;

(v) Hakikisha umejaza vizuri dodoso juu ya taarifa mbalimbali kuhusu janga kwenye mkataba wa bima;

(vi) Lipa ada na tozo za bima yako katika muda uliotakiwa ili kukamilisha bima inayokusudiwa; na

(vii) Hakikisha umepata mkataba wa bima toka kwa kampuni ya bima ambao utakuwa ushahidi sahihi juu ya bima yako hata wakati wa ajali au kudai fidia endapo janga litatokea.

**JINSI YA KUDAI FIDIA YA BIMA**

(i) Mara tu janga lililokatiwa bima likitokea kwa mfano ajali, mjulishe mtoa bima wako yaani dalali, wakala au kampuni ya bima ulikochukua bima;

(ii) Dalali, wakala au kampuni ya bima itakuongoza hatua za kufuata ili kulipwa fidia husika;

(iii) Hakikisha umejaza fomu ya madai kikamilifu kulingana na maelezo ya awali yaliyopo kwenye mkataba wa bima;

(iv) Wasilisha nyaraka zote husika kwa kampuni ya bima kadri ulivyoongozwa na dalali, wakala au kampuni ya bima wakati unatoa taarifa ya janga lililotokea; na

(v) Kampuni ya Bima itakufidia kulingana na sheria au miongozo iliyowekwa kwenye kampuni husika.

> Wakati mwingine mtu hukatia bima nyumba bila kuweka bima ya vifaa au vitu mbalimbali vya thamani vilivyo ndani ya nyumba hivyo ni vizuri kutambua aina ya bima unayochukua kulingana na mahitaji.

**HATUA ZA KUFUATWA KATIKA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO**

Kama hukuridhika na hali halisi ya ushughulikiaji wa madai yako yoyote kwa kampuni ya bima, dalali au wakala unaweza kuwasilisha malalamiko yako kwa kamishina wa TIRA. Ifahamike malalmiko ni lazima yaletwe kwa njia ya maandishi na kuambatishwa vielelezo sahihi.

Endapo, malalamiko yako ulishayawasilisha katika moja ya Mahakama, malalamiko hayo hayawezi kushughulikiwa na kamishina wa TIRA ili kuepuka kuingilia muhimili wa mahakama. Inashauriwa kuhakikisha kuwa kampuni unayotaka kupata huduma za bima iwe imesajiliwa kisheria na inatambulika na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

Taarifa zaidi kuhusiana na bima zinapatikana kwenye tovuti ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania www.tira.go.tz pia unaweza kuwasiliana kupitia barua pepe coi@tira.go.tz



# Hedhi salama

*inatoka uk.14*

Lakini mimi naongeza kwamba elimu hii asiipate mtoto wa kike peke yake bali pia wavulana na wanaume. Hawa pia wakiipata kisawasawa, jambo linakuwa jepesi.

Kwa mfano, zamani suala la kliniki lilikuwa likimhusu mwanamke pekee kwa sababu iliaminika kwamba ndiye mtu sahihi kwa sababu ndiye anazaa. Lakini ikaja kugundulika kwamba mumewe pia ni muhimu kuambatana na mkewe kwenda kliniki na kusikia maelezo ya daktari na hasa kwa kuzingatia kwamba katika jamii zetu bado mume ndiye mtoa maamuzi.

Kwa mfano, mwanamke mjamzito anapokwenda kliniki peke yake, daktari akampima na kumwambia kwa jinsi mimba yako ilivyo, hutakiwi kufanya kazi na muda mwingi unatakiwa kulala (bed rest), pia unatakiwa kula matunda kwa wingi, mayai ya kuku wa kienyeji (ambayo ni ghali kwa maeneo kama Dar es Salaam) na mbogamboga na maini kwa wingi ili kupata madini chuma yatakayokusaidia kutengeneza damu kwa wingi mwililini.

Unadhani ni wanaume wangapi hasa wenye dalili ya ubahili na chembechembe za mfumo dume kwenye damu zao watamwelewa mwanamke huyu? Watahisi amejitungia ili asifanye kazi, ana deka na anasingizia daktari ili awe anakula kile kitu roho inapenda! Lakini kama wanaume wanamsikia daktari mwenyewe anazungumza, hawawezi kuwa na mawazo ya aina hiyo.

Vivyo, elimu ya hedhi ni muhimu pia kwa watoto wa kiume na wanaume na kwa mfano huo najua sasa kwa nini ninaona ni muhimu watoto wa kiume pia wanapata elimu hii.

Waziri Ummy amesema kila mwezi wanawake bilioni 1.9 wanakuwa katika kipindi cha hedhi kati ya watu bilioni 7 waliopo duniani, ambayo ni asilimia 26, wengi wakiwa ni wenye miaka 15-49.

Aidha Tanzania kwa mujibu wa takwimu za watu na makazi zilizotolewa mwaka 2022 na Ofisi ya Takwimu (NBS), wanawake milioni 14.9 hupata na changamoto ya hedhi salama hususan wale walio na umri wa miaka 15-49.

"Idadi hii ni kubwa hatuwezi kudharau mahitaji yao, hatuwezi kukaa kimya. Huu ni wajibu wetu kupata hedhi salama kuanzia ngazi ya kaya, taasisi mpaka jamii," ameeleza Waziri Ummy.

Nini tatizo tunapokuwa na hedhi isiyo salama? Majibu ni mengi ambapo kwa wanafunzi ni kuchangia hata kuzorotesha maendeleo yao darasani.

Waziri Ummy amesema Taasisi ya Utafiti ya Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ilifanya utafiti ambapo asilimia 17 ya wasichana walishindwa kuhudhuria masomo kutokana na maumivu ya tumbo, kuogopa fedheha endapo wangechafuka na kukosa vifaa salama.

"Ni matumaini yangu leo tunapozindua maadhimisho ya Hedhi Salama itakuwa ni chachu kuwekeza kwenye miundombinu na vifaa ili kuwafanya wahudhurie mashuleni," amesema Waziri Ummy.

Lakini athari kubwa ya kiafya kwa kutokuwa na hedhi salama ni idadi kubwa ya wanawake kupata uambukizo katika njia ya mkojo (UTI).

Kimsingi ninachosema hapa ni kwamba hedhi salama ni jambo la lazima. Ni muhimu elimu kuhusu suala hili itolewe na wazazi na mamlaka nyingine bila kikwazo. Hatuna sababu ya kuona jambo hili kama kinyaa au mwiko kulizungumza.

Huduma katika mazingira ya vyoo hususani mashuleni ziimarishwe kwa kuweka pia vyumba usiri, uwepo maji ya kutosha, vifaa salama na utupaji salama wa vifaa vilivyotumika.

Ni vizuri taasisi mbalimbali na watu wenye mapenzi mema kwa mabinti zetu na Mwenyezi Mungu amewajaalia kuwa na kipato, kujenga utaratibu wa kutoa bure taulo za usafi mashuleni mara kwa mara, hususani shule za Vijijini.

Haiwezekani mambo niliyokuwa ninayaona miaka ya 70, kipindi ambacho neno kompyuta tulikuwa tunalisoma kama kitu cha kusadikika na kisichotuhusu, yaendelee kuwa yaleyale katika zama hizi za matumizi ya akili mnemba.

# Kazi pevu za Samia



**Rais Samia Suluhu Hassan akipongezwa baada ya kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba mjini Dodoma.**

*inatoka uk.15*

Pia mbali na kufanya kazi serikalini na katika shirika hilo la Umoja wa Mataifa, Dk. Samia alipata kufanya kazi na taasisi zisizo za kiserikali kwa miaka karibu kumi akijikita zaidi katika harakati za usawa wa kijinsia.

Alijiunga rasmi na siasa mwaka wa 2000 wakati alipochaguliwa kwenye Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kama Mjumbe Maalumu. Kuingia kwake kwenye siasa kuliifanya nyota yake kuanza kuchomoza katika medani za kisiasa na uongozi ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baadaye akateuliwa kuwa Waziri wa Afya, Jinsia na Watoto; uteuzi uliofanywa na Rais wa kipindi hicho Aman Abeid Karume.

Mwaka 2005 alichaguliwa tena kuwa mjumbe maalumu na kuteuliwa upya kama Waziri, wakati huu akipewa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji katika Serikali ya visiwani. Mwaka wa 2010 alitia nia ya kuwania uwakilishi ambapo alichaguliwa kuwa mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi huko Zanzibar.

Nyota ya Dk. Samia ilivuka mipaka kwani muda mfupi baada ya uchaguzi mkuu wa 2010 alichomoza kwenye Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuteuliwa na aliyekuwa Rais wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Waziri wa nchi anayeshughulikia masuala ya Muungano katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihudumu chini ya Makamu wa Rais wa wakati huo, Dkt. Mohamed Gharib Bilal.

Machi mwaka 2014 Tanzania iliingia kwenye vuguvugu la kubadili Katiba yake ambapo huko nyota ya Rais Samia ilichomoza tena baada ya kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba mjini Dodoma.

Dk. Samia alichaguliwa kwa kura 390 sawa na asilimia 74.6 na kumshinda mpinzani wake Amina Abdalla Amour ambaye alipata kura 126 sawa na 24%. Atakumbukwa sana wakati wa Bunge la Katiba, kwani ndipo alipoanza kutabiriwa kushika nafasi ya juu zaidi ya kiutawala ambapo mmoja wa wajumbe aliwaasa wajumbe wamfikirie Mama Samia kwa nafasi ya juu zaidi kwenye uchaguzi uliokuwa unafuata wa mwaka 2015.

Nyota ya Dk. Samia Suluhu haikuwahi kuzimika wala kufifia kwani Julai mwaka 2015, Dk. John Magufuli mara baada ya mpambano mkali ndani ya CCM uliompa ushindi wa kupeperusha bendera ya CCM kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka huo, mbele ya wajumbe wa mkutano Mkuu alimpendekeza Mama Samia kuwa mgombea mwenza wake.

Hatimaye baada ya uchaguzi Dk. Samia aliweka historia nyingine ya kupanda katika siasa za Tanzania kwa chama chake kupata ushindi kwenye uchaguzi mkuu uliomuweka yeye katika historia nyingine ya kuwa msaidizi mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana ya Makamu wa Rais akiwa ni mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo.

Mwaka 2020, aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati John Magufuli wakati akiomba ridhaa ndani ya chama chake ili apeperushe tena bendera ya CCM kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huo, kwa mara nyingine alimpendekeza Dk. Samia kuwa mgombea mwenza wake ambapo ushindi wa chama chake uliilinda historia ya Dk. Samia.

Baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Pombe Magufuli, katiba ilimlazimu Dk. Samia kuwa Rais wa Tanzania na kuweka historia nyingine ya Rais wa kwanza wa mwanamke Tanzania.

Wapo waliomtilia shaka kutokana na jinsi yake lakini aliwahakikishia Watanzania baada ya ile kauli aliyoisema Dodoma baada ya kuapishwa; "Huyu aliyesimama hapa ni Rais mwenye maumbile ya kike, lakini ndiye Rais wa Tanzania kwa sasa."

Tangu hapo amedhihirisha kwamba, jinsia ni maumbile tu! Lakini uwezo wa kufanya kazi kati ya wanaume na wanawake hautofautiani kabisa!

Dk. Samia hakuna cha kumzuia kugombea na kushinda Uchaguzi mkuu wa mwakani tena asubuuuuhi.

Kilichobaki ni kudura tu za Mwenyezi Mungu kumpa uhai Rais wetu ili mwakani tumchagure sisi wananchi kupitia sanduku la kura, baada ya kufanya vizuri sana. Hakika Mwenyezi Mungu anatupenda Watanzania kutupa Rais muungwana sana.

***Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 au 0784 122 020.***



**Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na hayati John Pombe Magufuli.**

# Wajificha vichakani kwa hofu ya kutekwa nyara

**ABUJA, Nigeria**

BAADHI ya watu walionusurika katika tukio la karibuni la utekaji nyara wa watu wengi Kaskazini mwa Nigeria, wameambia BBC kwamba wanahofia maisha yao.

Takriban watu 10 waliuawa na wengine 160, wengi wao wanawake na watoto, walitekwa nyara Ijumaa iliyopita katika Kijiji cha Kuchi Jimbo la Niger.

Mkazi mmoja aliambia BBC kwamba watu sasa wanajificha vichakani, baada ya wavamizi wengine kurejea Jumapili usiku.

Mke wa Jubril, alikuwa akirudi kutoka katika nyumba ya baba yake Ijumaa jioni alipotekwa.

"Nina huzuni. Inasikitisha sana. Wakati wowote wanaweza kurudi. Watu waliobaki wanajaribu kujificha vichakani." Kamishna wa Usalama wa Ndani wa Jimbo la Niger, Muhammed Bello, alisema idara yake, pamoja na vyombo mbalimbali vya usalama, vinachunguza utekaji nyara huo, ingawa amepinga idadi ya watu waliochukuliwa.

"Kwa kweli haimaanishi kwamba wote wamechukuliwa na waasi au majambazi, baadhi yao huenda wamekimbilia msituni au kuvuka maji kwa sababu ya mkanganyiko."

Kamishna huyo alisema serikali inafanyia kazi mpango wa mashirika mbalimbali ili kukabiliana na ongezeko la idadi ya mashambulizi.

"Tunashirikiana kwa hivyo tuna operesheni hizi za kijeshi zinazofanyika katika majimbo kwa wakati mmoja, kwa hivyo hakutakuwa na njia ya kutoroka kwa yeyote kati yao," alisema.

Hata hivyo, wakosoaji wanaishtumu serikali kwa kushindwa kuzuia mashambulizi, ambayo yamekithiri



katika majimbo ya kaskazini.

Akizungumza kwa niaba ya mgombea urais wa chama cha Labour Peter Obi, Dk. Yunusa Tanko, aliambia BBC kuwa ongezeko la idadi ya utekaji nyara katika maeneo fulani, si la kushangaza kwa sababu ya kile alichoeleza kuwa kupuuzwa kwa serikali za mitaa katika maeneo ya mashambani.

Shirika la Kutetea Haki za Binadamu la Amnesty International lilisema lina wasiwasi mkubwa juu ya utekaji nyara wa watu wengi, likisema ni dalili nyingine ya kushindwa kabisa kwa mamlaka ya Nigeria kulinda maisha.

Katika kipindi cha mwezi uliopita, vijiji kadhaa vilivamiwa na magenge yenye silaha ambayo yanawateka nyara ili kujipatia fidia.

Mara nyingi haijulikani ikiwa watu hao wenye silaha, wana uhusiano wowote na makundi ya kijihadi.

BBC.

# Netanyahu aapa kuendeleza vita

**YERUSALEM, Israel**

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, ameapa kuendeleza vita dhidi ya Hamas licha ya kukosolewa kimataifa kuhusu shambulizi la anga lililoua Wapalestina wengi mjini Rafah Jumapili iliyopita.

Takriban watu 45 waliuawa, kwa mujibu wa Wizara ya Afya inayoendeshwa na Hamas, huku mamia ya wengine wakipatiwa matibabu kutokana na majeraha ya moto.

Akizungumza katika Bunge la Israel, Waziri Mkuu, Netanyahu alisema shambulizi hilo lilikuwa msiba mbaya, lakini akaongeza: "Sina nia ya kumaliza vita kabla ya kila lengo kufikiwa."

Alisema ni muhimu Israel kufanya kila juhudi kuwalinda raia na kusisitiza kuwa Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) linatumia juhudi zao bora zaidi kutowadhuru wale wasiohusika katika mzozo huo.

Hotuba ya Netanyahu ilikatizwa



na hekaheka za mara kwa mara kutoka kwa jamaa za mateka waliochukuliwa na Hamas wakati wa shambulio la Oktoba 7, mwaka jana ambao baadhi yao wamekuwa wakimkosoa kwa kushindwa kufanya makubaliano ya kurejeshwa kwa wapendwa wao.

"Huko Rafah tayari tumeahamisha takriban wakazi milioni moja wasio wapiganaji na licha ya jitihada zetu kubwa za kutowadhuru wasio wapiganaji, kwa bahati mbaya kitu kilienda vibaya, alisema Netanyahu. BBC.

# ...Baraza la Usalama la UN laitisha kikao cha dharura



**WASHINGTON, Marekani**

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) lilitarajiwa jana Jumanne kufanya mkutano wa dharura kwa ombi la Algeria, kujadili mgogoro wa Rafah.

Katika taarifa yake juzi Jumatatu, Katibu Mkuu wa UN, António Guterres, alisema shambulizi hilo limeua raia wengi wasio na hatia ambao walikuwa wakitafuta tu hifadhi kutokana na mzozo huo mbaya.

"Hakuna mahali salama Gaza. Hofu hii lazima ikomeshwe," alisema.

Israel inaendelea kukumbwa na wimbi la shutuma kutoka jumuiya ya kimataifa kuhusiana na shambulizi hilo.

Maafisa wa afya wa Gaza walisema watu 45 waliuawa katika shambulizi la angani la Israel katika kambi ya wakimbizi.

Shambulizi hilo lilisababisha moto mkubwa katika kambi ya wakimbizi wa Kipalestina.

Israel kupitia Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu, imesema inachunguza tukio hilo lililoliita ajali ya kusikitishwa na athari zake kwa raia.

Jeshi la Israel lilisema shambulizi hilo la Jumapili usiku Kusini mwa Rafah, liliwalenga na kuwaua maafisa wawili waandamizi wa Hamas, lakini pia likasababisha moto ambao Wapalestina na nchi nyingi za Kiarabu, zimelaani kwa kuliita tukio hilo ni la mauaji ya kikatili.

Msemaji wa Baraza la Usalama wa Kitaifa la Marekani, alisema Israel lazima ichukue tahadhari zote kuwalinda raia. Mjumbe wa Umoja wa Mataifa katika Mashariki ya Kati, Tor Wennesland, ameitaka Israel kufanya uchunguzi wa kina na wa wazi kuhusu tukio hilo. DW.

# Zelensky awataka viongozi wa Magharibi kuishinikiza Urusi

**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amewataka viongozi wa nchi za Magharibi kuishinikiza Urusi kuingia katika amani kwa kutumia njia zote zinazohitajika.

Akizungumza nchini Uhispania, Rais Zelensky alisema kuna haja ya kuwa na shuruti inayoonekana ya Urusi ambayo ilikuwa inataka kuharibu Ukraine na kusonga mbele.

Rais Zelensky amekuwa akisema kwa muda mrefu hatajadiliana na Urusi moja kwa moja hadi majeshi ya Moscow yaondoke katika maeneo yote ya Ukraine, ikiwa ni pamoja na Crimea.

Wito wake, hata hivyo, unakuja wakati Urusi inapata mafanikio dhidi ya Ukraine, huku Kyiv ikikabiliwa na uhaba wa silaha zinazotolewa na nchi za Magharibi.

Rais Zelensky alisema Urusi ilikuwa ikidondosha mabomu 3,200 ya angani yaliyokuwa yakiongozwa dhidi ya Ukraine kila mwezi.

"Unapambanaje na hilo?" Aliwauliza waandishi wa habari mjini Madrid ambapo alikutana na Waziri Mkuu, Pedro Sánchez.

Kiongozi huyo wa Ukraine alikataa wazo la kuialika Urusi kwenye mkutano wa kilele wa amani uliopangwa kufanyika nchini Uswizi mwezi ujao.

Mkutano huo unatarajiwa kujumuisha wawakilishi wa zaidi ya nchi 90.

Msemaji wa Kremlin, Dmitry Peskov, alisema Rais wa Urusi, Vladimir Putin, yuko tayari kwa mazungumzo, lakini kufikia malengo ambayo sasa yanafikiwa kupitia operesheni maalum ya kijeshi, kama Urusi inavyoelezea vita vya Ukraine.

Mjini Madrid, Rais Zelensky aliwataka viongozi wa nchi za Magharibi kuondoa marufuku ya silaha zilizotolewa kutumika kushambulia eneo linalotambulika kimataifa la Urusi.

Nchi nyingi za Magharibi ikiwa ni pamoja na Marekani, zimesisitiza kwamba Kyiv inalenga mashambulizi yake kwa vikosi vya Kirusi vinavyokalia eneo la Ukraine.

"Tunahitaji kufanya kazi pamoja na kuweka shinikizo siyo tu kwa Urusi, lakini pia kwa washirika wetu kutupa fursa ya kujilinda dhidi ya Urusi," Kiongozi huyo wa Ukraine alisema.

Moja ya masharti ya kupokea msaada wa mabilioni ya pauni kutoka kwa washirika wa Magharibi, ni kwa Kyiv kuelezea maono yake ya jinsi vita hivi vinapaswa kumalizika. BBC.



# Unaikumbuka bendi ya Sosoliso ya Congo?

## ●Ilitikisa Afrika Mashariki kwa vibao vyake murua

**Na Hamid Yassin**

BENDI ya Trio Madjes 'Sosoliso' ilikuwa imesheheni vijana na kuweza kulitikisa Jiji la Kinshasa huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika medani ya muziki.

Chanzo cha kuanzisha bendi ya Trio Madjes (Sosoliso), kulitokana na kuporomoka kwa bendi ya Orchestra Veve baada ya wanamuziki wake wengi kuikacha bendi hiyo.

Mwanamuziki Kiamungwana Wazolambongo 'Verckys', alikuwa kiongozi wa bendi hiyo ya Orchestra Veve iliyotamba mwanzoni mwa miaka ya 1970. Sifa kubwa ya Verkys alikuwa bingwa wa kulipuliza saxophone, hivyo kupelekea watu mbalimbali kumsifu mwanamuziki huyo kuwa na mapafu ya chuma.

Bendi ya Orchestra Veve iliwahi kutamba na nyimbo kama 'Baluti', 'Vivita', 'Nakoma Juste', 'Ndona' na 'Kalala.'

Lakini kitu kikubwa ambacho kilisababisha kuporomoka kwa bendi ya Orchestra Veve, ilikuwa ni baada ya waimbaji wake mahiri kuondoka katika bendi hiyo na kuanzisha bendi yao ambayo waliipa jina la Trio Madjes 'Sosoliso' . Baadhi ya waimbaji hao walikuwa ni Matadidi Buana 'Kitoko', Djeskin Loko 'Masengo' na Tshekabu Saak 'Sakoul.'

Pamoja na uchanga wa bendi ya Trio Madjes, lakini bendi hiyo iliweza kupata umaarufu mkubwa mara baada ya kuanzishwa kwake. Wakiwa katika bendi hiyo walitengeneza nyimbo kabambe zilizokuwa tishio kwa bendi kubwa za Kinshasa. Nyimbo hizo zilikuwa ni 'Bibie', 'Mousa', 'Sonie', 'Pambeni', 'Photo ya Madjesi', 'Toboye Africa', 'Matadidi' na 'Shery Nnuter.'

Bendi ya Trio Madjesi iliweza kufanya maonesho yake katika kumbi mbalimbali za starehe na kujaza mashabiki wengi. Miongoni mwa kumbi hizo zilikuwa ni Place de la Voix du Zaire. Inasemekana kwamba, wa ghafla waliokuwa wakipata hawa vijana wa bendi ya Trio Madjesi. Wakaapa kulimaliza kundi hilo, hasa pale kundi hilo lilipopata mwaliko wa kukaribishwa katika Mji wa Paris na kufanya onesho lao katika ukumbi wa Olympia.


Siku moja Trio Madjesi wakakaribishwa kwenye onesho walilolifanya Bangui nchini Chad. Walipolipwa fedha zao kwa pesa ya Kifaransa, wakaamua kubadilisha fedha zao kuwa za Zaire kwa njia ya magendo badala ya kutumia benki ya Zaire ili wapate fedha nzuri, jambo ambalo lilikuwa ni kosa la jinai.

Baada ya bendi ya Trio Madjesi kubainika kutenda kosa ilo, bendi hiyo ikapewa adhabu ya kutofanya shughuli za muziki kwa miezi sita. Huo ndio ukawa mwanzo na mwisho wa bendi ya Trio Madjesi.

kuna siku bendi ya Trio Madjesi ilipokuwa ikifanya moja ya onesho lake, kuna kundi la mashabiki ambao walikuwa wamepanda juu ya paa la Kanisa la Mtakatifu Andrew maeneo ya Mature, ili wawaangalie onesho hilo, lakini Paa la Kanisa lilivunjika na baadhi ya mashabiki wakajeruhiwa na wengine kupoteza maisha.

Hata hivyo wakongwe wa muziki wa Kongo hawakufurahia umaarufu















# Schwarzenegger: Ningekuwa rais mzuri wa Marekani



**LOS ANGELES, Marekani**

NI saa tano asubuhi mjini London na Arnold Schwarzenegger ni mtu anayejua watu wanataka nini. Ninapouliza ikiwa mgomo wa waigizaji unaoendelea unamaanisha kwamba mimi nitalazimika kufanya tungo zake anazozifahamu zaidi, hakusita kujieleza.

Mwigizaji huo wa filamu maarufu za Predator na Terminator anasema kwa hamaki: "Mgomo wa waigizaji unawakataza kutangaza sinema zenu, lakini si lazima nizikuze.".

Hata akiwa na umri wa miaka 76, Schwarzenegger si mtu ambaye unaweza kubishana naye kuhusu maandishi madogo ya chama cha wafanyakazi. Hapa ndipo hatua ya mgomo inapokutana na shujaa wa vitendo.

Tumeketi kwenye madawati karibu ya ukumbi wa michezo tukirekodi mahojiano ya BBC Breakfast katika kituo cha Mafunzo ya Kibinafsi cha Walinzi, kilichoko Bungeni Hill Lido, na tunapata nafasi hiyo. "Mazoezi bora kuliko niliyokuwa nayo asubuhi ya leo Claridge," anaongeza kusema kwa shauku, huku pia akinijulisha kwamba leo tayari amefanya mazoezi.

Mpiga picha wangu Peter ameandika Arnold Schwarzenegger kwenye ubao wake wa kupiga makofi na kumgeukia, akiuliza kwa wasiwasi: "Tafadhali niambie niliandika jina lako kwa usahihi?"

Ninaweza kuthibitisha kwamba inamchukua hata Arnold Schwarzenegger sekunde mbili kamili kutahajia jina lake mwenyewe, kabla hajatazama juu na kutabasamu: "Ndiyo."

Ishara moja baadaye na mahojiano yanaweza kuanza.

Arnold Schwarzenegger yuko London kuzungumzia kitabu chake kipya Be Useful: Seven Tools for Life, ambacho kinapokelewa vyema katika sehemu zisizotarajiwa. The Guardian haijulikani kuwa karibu na wanasiasa wa Republican, lakini ukaguzi wake ulihitimisha: "Mwongozo ambao unafanya kazi kweli."

Gazeti la Los Angeles Times lilimuangazia kwa shauku kidogo, "Maandishi hayafanyi kazi nyingi," huku likiendelea kukiri: "Je, nilijitahidi zaidi baada ya kusoma kitabu? Unaweza kuweka dau."

Na hivyo ndivyo hasa Arnold ("Anapendelea Arnold kuliko Arnie", mlinzi wake alitudokeza kabla hajafika) anachotarajia kufikia na kitabu hicho.

Sura hizo saba ni pamoja na Work Your Ass Off, Never Think Small and Shut Your Mouth Open Your Mind. (Fanya Kazi Kwa Bidii, Usiwe na Usiwe Fikira ndogo na Funga Kinywa Chako Fungua Akili Yako.

"Wazo nyuma yake ni kwa watu kuwa na mafanikio zaidi," anafafanua.

"Ilikuwa moja ya mambo ambayo sikuwahi kutamani, kuwa mzungumzaji wa kutia watu motisha, au kuandika vitabu vya motisha, kwa sababu nilipokuwa mkubwa nilitamani tu kuwa mtu mwenye misuli zaidi duniani," anasema mwigizaji huyo bora mara saba na wa tuzo ya mshindi wa Mr Olympia na Mr Universe mara nne, kabla ya kujiimarisha: "Na kuingia kwenye sinema na kutengeneza mamilioni ya dola."

Mambo yalibadilika ingawa baada ya miongo miwili ya filamu kali , zikiwemo Conan the Barbarian, Twins and True Lies,

Ghafla akawa na "ndoto mpya" na "malengo mapya" na akagundua kwamba: "Watu walihitaji sana kuhamasishwa na walikuwa wakinitazamia kupata majibu. Walistaajabia nilichokuwa nimetimiza, na ndipo nikapata wazo la kuandika kitabu hiki."



Ninauliza ikiwa kujisaidia ni neno chafu na jibu lake linafichua kile anachoamini kuwa ni dhana potofu ya kawaida juu yake: "Tunahitaji mchanganyiko wa kujisaidia, lakini pia kupata msaada kutoka nje. Siku zote huwa nachukia watu wanaposema mimi, 'Wewe ni maelezo kamili ya mtu aliyejitahidi mwenyewe kufikia malengo yake maishani.'

"Nachukia hilo," anarudia kwa nguvu zaidi.

"Sitaki mtu yeyote afikiri kwamba anaweza kufanya hivyo mwenyewe. Sote tunahitaji msaada."

Ifuatayo ni orodha ndefu ya watu, bila msaada na msukumo ambao Schwarzenegger anasema hangefanikiwa. Watu hao ni pamoja na Reg Park, mjenga misuli aliyezaliwa Leeds ambaye aliigiza katika filamu za Hercules za miaka ya 1960, hadi "watu milioni 5.8 walionipigia kura", akimaanisha mihula yake miwili kama gavana wa Republican wa jimbo la California.

"Ninaelezea katika kitabu kwamba tunapaswa kuwatambua wote waliokusaidia na mara tu unapogundua hilo, basi unatambua ukweli kwamba umepata pia kusaidia watu wengine."

Kuwasaidia wengine ni jambo ambalo Schwarzenegger amefanya kwa miongo mitatu iliyopita; kutoka kujihusisha na Michezo Maalum ya Olimpiki, hadi kutoa dola milioni moja kwa washiriki walio mstari wa mbele wakati wa majanga na kuandaa karamu ya chakula cha jioni ya Oktoberfest mapema mwezi huu, ambayo ilichangisha dola milioni saba kwa ajili ya programu yake ya vilabu vya baada ya shule.

### Siku ya hukumu kwa kweli

Schwarzenegger anataka watu wajue kwamba ingawa amefanikiwa maishani, yeye pia amepata shida.

"Kulikuwa na hali ya kushindwa kwa kiasi kikubwa na hasara kubwa," anakiri, kabla ya kuelezea mashindano ya kujenga misuli ambapo alipigwa kwenye filamu ambazo zilihusisha kuigiza kushambuliwa na mabomu.

"Na hata kumekuwa na hasara za kibinafsi kama ndoa yangu," anaendelea, akionyesha nia ya kuwa hatarini, ambayo ilionekana kuwa haiwezekani kwani aliua watu 77 katika eneo moja kwenye kilele cha filamu ya Comando.

Kitabu cha Be Useful hakiijumuishi maelezo ya mambo ya nje ya ndoa, ikiwa ni pamoja na kumpachika kijakazi huyo mimba, ambayo ilisababisha talaka yake na mpwa wa John F Kennedy, Maria Shriver. Alishughulikia yote hayo katika wasifu wake wa mwaka 2012, Total Recall. Hata hivyo inafichua jinsi alivyojikwamua kutoka kwa changamoto za kibinafsi anaelezea katika utangulizi wa kitabu kama "ulimwengu unaomzunguka".

"Lazima uwajibikie makosa yako. Huwezi kumlaumu mtu mwingine kwa hilo. Chukua jukumu. Kubali makosa na ujifunze kutokana na hilo kisha utafute namna ya kuwa mtu bora."

Pamoja na mafanikio yake yote kuna jambo moja ambalo Arnold Schwarzenegger hatawahi kuwa rais wa Marekani.

Katiba ya Marekani inasema kwamba mtu yeyote anayeshikilia wadhifa huo lazima awe raia wa kuzaliwa. Schwarzenegger anatokea Thal, Austria, ambako aliishi hadi umri wa miaka 19.

Ninamuuliza ni kero kiasi gani anapata kutostahili kwake.

"Ninahisi kama ningekuwa rais mzuri," anasema bila kuonyesha mashaka hata kidogo, kabla ya kuendelea: "Lakini ninahisi kwamba, wakati huo huo, kila kitu ambacho nimekamilisha ni kwa sababu ya Amerika.

"Marekani ilinipa fursa nyingi sana na watu wa Marekani walinikubali, na walinipokea kwa mikono miwili. Hakukuwa na mtu ambaye alinizuia kutoka kwa mafanikio yangu.

"Kwa hivyo kitu pekee ambacho siwezi kufanya, ni kugombea urais, sitalalamika juu ya hilo."



# Hakuna kisichowezekana, tuwekeze kwenye soka letu



Edson Arantes do Nascimento 'Pele'

**Na Hamid Yassin**

NIMEMKUMBUKA shabiki mmoja wa soka nchini Brazil alivyolalamika mwaka 1994, akihoji kwa nini Brazil haijamzaa Edson Arantes do Nascimento Pele mwingine!

Pamoja na ukongwe wangu, sikubahatika kumuona Pele akicheza mubashara, lakini nilisikia kila kitu juu ya nyota yule na kushuhudia klipu za video zake ambaye hivi sasa ameshatangulia mbele ya haki. Na nilielewa Mbrazil yule aliyekuwa akilalamika alimaanisha nini.

Siyo tu ilikuwa raha kumwona Pele aliyevaa jezi namba 10 akiingia uwanjani, bali pia ilikuwa burudani ya kutosha na uhakika wa ushindi hata kabla ya kuona ama kujua kile atakachofanya.

Pele alipendeza kuanzia namna alivyopokea mpira na namna alivyotoa pasi kwa wenzake achilia mbali chenga zake na magoli yake adimu.

Wengi tuliamini uchezaji wa Pele ulikuwa kipaji alichojaaliwa na muumba wake, lakini wao Wabrazil waliona tofauti, walisema Pele alitengenezwa akafikishwa pale na mfumo wa soka lao.

Walilalamikia ongezeko la rushwa nchini mwao kwamba limewaharibia soka hadi wamefikia kiwango cha kushindwa kumtengeneza Pele mwingine atikise dunia kisoka.

Wakati Wabrazil wakilalamikia soka lao, timu yao ya Taifa ndiyo ilikuwa bingwa wa dunia mwaka 1994 na ndiyo iliyotoa mchezaji nyota aliyeitwa Romario de Souza Faria.

Lakini wao bado hawakuridhika walilalamikia Brazil kucheza fainali kwa dakika 120 pia walilalamikia kuutwaa ubingwa kwa Penati. Waliona penati ya Robert Baggio mchezaji wa Italia iliyopaa iliwapa ubingwa usiostahili wao kujivunia duniani, walitaka ubingwa unaopatikana ndani ya dakika tisini na unaotokana na magoli yao ya kufunga siyo goli la kukosa litokalo kwa mchezaji wa timu pinzani.

Huo ndio utamaduni wa watu makini kwa lile wanalolipenda, lazima wawe na vigezo vyao vinavyowawezesha kujipima pia wawe na historia ambayo wakiirejea yaani wakitazama nyuma walikotoka wanajua kama wanasonga mbele ama wanadorora.

Wakati mashabiki wakiombolezea soka la Brazil lililouawa na rushwa na kusababisha nchi yao ishindwe kumtengeneza nyota wa kung'ara na kuifunika dunia, hali haiko tafauti na mataifa mengine dunia ikiwemo nchi yetu ya Tanzania.

Hadithi ni ile ile kama Brazil na Pele, hata sisi achilia mbali soka hata kwenye michezo mingine tunawaimba na kuwasifu sana wanamichezo wetu wa miaka ya sabini kuliko kizazi cha sasa!

Wenyewe wa kizazi cha sasa hawakubali hili, wanasema 'mnawapakulia minyama' wachezaji wa zamani lakini hakuna walichofanya hususani kwenye soka!



Rais wa TFF, Wallace Karia

Wanasema wachezaji wa kizazi cha sasa cha soka wamefuzu Kombe la Mtaifa ya Afrika mara mbili wakati wale wa zamani wanaosifiwa walishiriki mara moja tu mwaka 1980! Ni kweli wanachosema lakini lazima watambue hiyo imetokea kwenye mazingira tafauti.

Timu ya Taifa iliyokwenda kucheza fainali ya Mataifa Huru ya Afrika (sasa hivi AFCON) mwaka 1980 wakati ule timu zilizocheza fainali ile zilikuwa nane tu miongoni mwa mataifa yote ya Afrika.

Yaani ilikuwa lazima upite vikwazo vingi maana timu zilikuwa zinacheza kwa mtindo wa mtoano mwanzo mwisho, hakuna cha makundi wala nini!

Hata baadaye ulipokuja mtindo wa kucheza hadi hatua ya makundi, ilikuwa lazima ushike nafasi ya kwanza kwenye kundi ndipo ufuzu hatua ya kucheza fainali za AFCON kwani timu shiriki zilikuwa 16 tu, yaani ni chache kuliko ilivyo sasa ambapo zimefikia 32!

Baada ya kuongezwa idadi ya timu za kucheza fainali za AFCON ndipo nasi Tanzania tumefanikiwa kushiriki mara mbili kupitia kushika nafasi ya pili kwenye hatua ya makundi mara zote mbili tulizofuzu.

Kwa hiyo habari kwamba wachezaji wa zamani walikuwa bora kuliko wa kizazi cha sasa inaweza kuwa na mantiki katika hilo.

Hata ngazi ya Klabu, huko miaka ya nyuma timu zetu zilitingisha katika soka la Afrika katika mazingira tafauti na ya sasa. Mwaka 1968 na 1969 timu ya Yanga ilifika hatua ya Robo Fainali ya Klabu Bingwa Afrika ikiwa imesheheni wachezaji wazawa tupu.

Tena mwaka 1969 ilitolewa kwa mizengwe ya maamuzi ya kumpata mshindi kwa njia ya kurusha shilingi, baada ya Yanga na Asante Kotoko ya Ghana kutoka sare ya bao 1-1 katika mechi tatu za nyumbani na ugenini na ile ya Uwanja Huru iliyofanyika Ethiopia!

Simba nayo ilifika nusu fainali ya Klabu Bingwa Afrika mwaka 1974 ikiwa na wachezaji wazawa watupu. Hii rekodi hadi leo haijavunjwa na timu yoyote ya Tanzania.

Mwaka 1998 Yanga ilifanikiwa kufuzu hatua ya makundi ya michuano ya Klabu Bingwa Afrika wakati huo ikishirikisha timu nane tu kwenye hatua hiyo ikiwa haina hata mchezaji mmoja wa nje ya Tanzania!

Watani wao wa jadi nao wakajibu mapigo mwaka 2003 walipofuza hatua ya makundi kwa kumtoa aliyekuwa bingwa mtetezi wa Afrika, Zamalek ya Misri ikiwa na mchezaji mmoja wa tu wa kigeni Mrundi



mwenye asili ya Congo DR, marehemu Ramadhani Waso.

Katika miaka ya karibu Simba imefika hadi robo fainali ya Klabu Bingwa Afrika mara nne na Kombe la Shirikisho mara moja lakini safari hii ikiwa imesheheni wachezaji wengi wa kigeni.

Yanga msimu huu nao wamefika hatua ya robo fainali tangu wafanye hivyo mara ya mwisho mwaka 1969, msimu uliopita walifika hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika kama walivyofanya mahasimu wao Simba mwaka 1993 ikiwa na wachezaji wote wazalendo!

Hivyo ukiangalia kwa makini hata soka letu tulikuwa tunafanya vizuri miaka ya nyuma kuliko hivi sasa ambapo tunategemea zaidi wachezaji wa kigeni kuzibeba klabu zetu kinyume na huko nyuma wazawa walipokuwa alfa na omega katika kila tu.

Miaka hiyo ya sabini wachezaji wengi walikuwa wanaibuliwa kupitia timu za vijana za kila klabu; mfano akina Sunday Manara, Juma Pondamali, Leodeger Tenga, Rishard Adolf, Mohamed Mkweche, Adulhamani Jafari, Kassimu Manara na wengineo kadhaa walipikwa pale Yanga ya vijana chini ya kocha Mkongo marehemu Tambwe Leya.

Kule Simba wachezaji kama akina Nicho Njohole, Abasi Kuka, George Kulagwa, Rahimu Lumelezi, Willy Mwajibe, na wengine kadhaa waliandaliwa tangu wakiwa wadogo kupitia Simba ya vijana chini ya kocha Mguine Nabi Kamara.

Kama miaka hiyo ya sabini timu zetu ziliweza kuandaa vijana wawe nyota wa baadaye wa klabu zao na taifa, kipi kinashindika hivi sasa wakati zama hizi kuna kila kitu kuanzia rasilimali fedha, viwanja vya kisasa, vitendea kazi kwa wingi sambamba na teknolojia mujarabu?

Au tunataka tuwe kama Brazil, kila ikivurunda inakumbuka zama za akina Pele, Gharincha, Tostao na nyota wao wengine wa miaka ile ya sabini? Tubadilike hakuna kisichowezekana!

**Kwa maoni na ushauri, 0768 888 787 ama 0784 122 020.**

# Je, Kombe la FA ndiyo mwisho wa Ten Hag Man United?

**MANCHESTER, England**

IKIWA meneja wa Manchester United Erik ten Hag ataondoka, basi baada ya kipindi chake kizuri kwa muda wake akinoa timu hiyo, na Kombe la FA likinyanyuliwa mbele ya maelfu ya wachezaji wa kikosi cha 'mashetani wekundu' kwenye uwanja wa Wembley, ni njia nzuri ya kuondoka.

Ten Hag alitumia muda wa maandalizi ya shindano hili la mwisho dhidi ya mahasimu washindi wa mashindano yote Manchester City, akiwa amegubikwa na uvumi kwamba huu ungekuwa mchezo wake wa mwisho, meneja asiye na chake akitembea, na kusubiri tu mmiliki mwenza mpya wa United, Sir Jim Ratcliffe kumpa shinikizo la mwisho.

Manchester City walikuwa hapa kumletea fedheha ya mwisho kabla ya kuondoka, na kutoa kipigo cha mwisho na kushuhudia kocha huyu akishindwa.

Badala yake, katika mojawapo ya michezo ya kupendeza inayojitokeza mara nyingi, Ten Hag alionyesha ustadi wa kuifunga Manchester City 2-1, Mholanzi huyo aliinua miguu yake juu katika kusherehekea firimbi ya mwisho na mlinzi shujaa Lisandro Martinez kabla ya kwenda kushirikishana naye tukio la kipekee, kumpa mkono wa faraja Pep Guardiola aliyechabangwa.

Kiwango cha mafanikio ya United wakati presha ilipokuwa juu zaidi kwa meneja na wachezaji ni kwamba hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa City kupoteza, mbali na mikwaju ya penalti dhidi ya Real Madrid katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa, tangu waliposhindwa na Aston Villa mnamo Disemba 6.

Iwapo hii inaleta tofauti yoyote kwa watoa maamuzi wa Old Trafford, wakiongozwa na Ratcliffe, bado ni jambo linalosubiriwa lakini kwa mateso yake yote na ukosoaji ambao amekumbana nao, mengi ya hayo yalihalalishwa baada ya msimu mbaya kama huo, Ten Hag alifurahia kipindi hiki akiwa Wembley.

Ratcliffe na muundo wake mpya wa kandanda hauwezekani kuunda mustakabali wa baadaye kwa kuzingatia mchezo mmoja, haijalishi ni wa sifa kiasi gani, na swali la msingi linaweza kuulizwa ni, imekuwa wapi United ambayo iliicharaza City, haswa mchezo wa kipindi cha kwanza kilichosisimua, kwa msimu wote huu?

Taarifa ya baada ya mechi iliyotolewa na Ratcliffe haikuwa vidokezo vyovyote kuhusu mustakabali wa Ten Hag lakini pia, haikutoa chochote cha msingi kwa umma, ambacho kilionekana muhimu.

Jibu la meneja huyo, kama ilivyokuwa siku zote, ni kusema kwa usahihi kwamba alirithi klabu na timu ambayo mtangulizi wake Ralf Rangnick alidai ilihitaji "upasuaji wa moyo".

Pia alitaja orodha ndefu ya majeruhi, akisema baada ya ushindi wa United: "Nawaambia hivi mwaka mzima. Wachezaji wanapokuwa sawa tunaweza kucheza soka nzuri sana. Huu ulikuwa mchezo mzuri sana dhidi ya timu bora zaidi duniani.

"Nadhani ukosoaji haukuwa wa haki, kwa timu na mimi pia. Haikuwa sawa. Hatukuwa na wachezaji. Tumeona mambo yale yale, ukosefu wa soka nzuri kila wakati – hapana, sio hivyo - lakini tulilazimika kujifinya kila wakati na matokeo yake, huwezi kucheza mpira unaotaka.

"Nilikuwa na kikosi kamili labda mara tatu au nne katika miaka miwili. Hata hapa tulikosa wachezaji wakubwa kama Harry Maguire, Luke Shaw na Casemiro.

Hoja zote ni sawa lakini zikidhoofishwa na ukosefu wa mkakati na udhibiti mara nyingi sana, na kampeni ya Ligi ya Mabingwa ambayo haikuwa na hadhi na sifa zake, United hata haikutoka katika hatua ya makundi.

Na hakika, United hawakutumia uzoefu na ustadi wao hadi kushinda Kombe la FA kwa mara ya 13.

Walipoteza uongozi wa mabao mawili kwa moja kabla ya kuilaza Newport County katika raundi ya nne na kupata ushindi



mkubwa wa 4-3 dhidi ya Liverpool katika robo fainali kwa bao la Amad Diallo katika sekunde za mwisho za muda wa nyongeza, kabla ya kuepuka aibu kubwa kwenye nusu fainali, ikiitoa kwa mabao 3-0 dhidi ya timu ya Championship Coventry City.

Ushindi huu wa kipekee dhidi ya mabingwa hao mara nne wa Ligi ya Primia ulikuwa wa kawaida lakini hakuna kilichobadilika katika mpangilio wa Ten Hag ambao uliwaletea mabao mawili muhimu kipindi cha kwanza.

Na ukweli kwamba walifungwa na vijana Alejandro Garnacho na Kobbie Mainoo utaleta furaha zaidi, kwa United, klabu ambayo daima imekuwa ikithamini vipaji vya vijana.

Bao la Mainoo lilikuwa la kipekee, krosi nzuri kabisa ya Marcus Rashford ikimpata Garnacho, ambaye krosi yake ilifikiwa na mguso mwembamba na kuona vizuri kwa Bruno Fernandes.

Mainoo, akiwa na umri wa miaka 19 pekee, alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mechi hiyo na kuonyesha ukomavu na udhibiti wa hali ya juu, na hivyo kudhihirisha kuwa ana tabia ya kucheza mechi kubwa dhidi ya wapinzani bora - ambayo itatiliwa maanani na meneja wa Uingereza Gareth Southgate kabla ya Euro 2024.

Pia unaweza kuona ilimaanisha nini kwa Rashford baada ya wiki mbaya ambapo kudorora kwake msimu huu kulitokana na uamuzi wa Southgate wa kumtoa fowadi huyo kutoka kwa kikosi cha muda cha wachezaji 33 cha England kwa ajili ya dimba la Ujerumani.

Rashford alitokwa na machozi wakati wa sherehe za United na mashabiki wao baada ya kukabidhiwa Kombe la FA.



Mmiliki mwenza wa Manchester United Sir Jim Ratcliffe akisalimiana na meneja Erik ten Hag baada ya ushindi wa fainali ya Kombe la FA

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Mei 29 - Juni 4, 2024 |

## Pep Gurdiola kutimka Man City



**MANCHESTER, England**

KOCHA Pep Gurdiola anatarajiwa kuondoka ndani ya Klabu ya Manchester City mwishoni mwa msimu ujao wa 2024/25 mara baada ya mkataba wake kumalizika.

Guardiola (52) aliyejiunga na Man City Mwaka 2016, amesaliwa na Miezi 12 katika mkataba wake na vyanzo vya Habari kutoka ndani ya klabu vinaeleza hataongeza mkataba mwingine.

Kocha huyo ambaye amebeba makombe 15 likiwemo la Ubingwa wa Ulaya, pia amebeba mataji 6 ya EPL ikiwemo kuweka rekodi ya kuwa kocha wa kwanza kubeba ubingwa huo mara nne mfululizo.

# Azam FC kucheza Klabu Bingwa Afrika

- Simba waambulia kucheza Shirikisho msimu ujao
- Geita Gold yaungana na Mtibwa 'Championship'
- Aziz Ki achukua kiatu cha dhahabu

**Na Waandishi Wetu**

AZAM FC imeichapa Geita Gold bao 2-0 na kung'ang'ania nafasi ya pili na kufanikiwa kukata tiketi ya kushiriki michuano ya Klabu Bingwa Afrika huku Simba iliyopata ushindi kama huo ikiambulia kupata nafasi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Simba iliyokuwa inahitaji ushindi kwa udi na uvumba kusaka nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu ya NBC, ilianza kipindi cha kwanza kwa mashambulizi ya moja kwa moja kwenye lango la JKT Tanzania, lakini papara za wachezaji wake ziliwaangusha kupata magoli.

Kadiri muda ulivyokuwa unaenda ndivyo Simba walizidi kupoteana uwanjani na kuwapa fursa JKT nao kuuchukua mchezo kwa kandanda safi la kuonana lakini umaliziaji mbovu wa wachezaji wake nao uliwaangusha kupata japo goli katika nafasi kadhaa walizozitengeza.

Kikwazo kikubwa cha JKT kupata goli alikuwa golikipa wa Simba, Ayoub Lackled aliyeokoa zaidi ya bao nne za wazi katika kipindi iko cha kwanza.

Kipindi cha pili JKT Tanzania waliamua kukaa nyuma kwa muda mrefu na kuwapa mwanya Simba ya kuwashambulia mfululizo hadi pale walipopata penalti iliyofungwa na Saidoo Ntibazonkiza dakika ya 86.

Willy Esomba Onana aliyeingia uwanjani kipindi cha pili akaifungia Simba bao la 2 dakika za majeruhi za kipindi cha pili.

Hata hivyo ushindi huo haukuiepusha Simba kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho msimu ujao baada ya Azam FC kupata ushindi kama huo na kung'ang'ania nafasi ya pili na itashiriki michuano ya Klabu Bingwa Afrika msimu ujao.

### Aziz Ki atwaa kiatu cha dhahabu

Mpaka mapumziko katika mechi ya Yanga dhidi ya Tanzania Prisons, mabingwa hao wa soka nchini walikuwa wanaongoza kwa bao 2-1, yote yakifungwa na kinara wao wa kufumania nyavu, Aziz Ki.

Prisons walikuwa wa kwanza kupata bao kupitia kiungo mshambuliaji wao kinda, Beno Ngassa dakika ya 9 ya mchezo.

Kipindi cha pili Yanga iliendeleza mashambulizi mfululizo hadi pale dakika ya 51 walipofanikiwa kupata bao la 3 kupitia Kennedy Msonda.

Dakika ya 78 mchezo Aziz Ki alijihakikishia kupata kiatu cha ufungaji bora baada ya kuifungia Yanga bao la 4 na la 21 kwake msimu huu. Hii pia ni 'Hat trick' ya pili kwake msimu.





Azam FC iliyokuwa inawania kubaki nafasi ya pili, nayo hadi mapumziko ilikuwa bado imebanwa mbavu na Geita Gold iliyokuwa inapigania roho yake isishuke daraja.

Kipindi cha pili Azam walirudi kwa kasi na kufanikiwa kupata bao la kuongoza lililofungwa na beki wao Mcolombia, Fuentes.

Feisal Salumu aliihakikishia Azam FC kucheza michuano ya Klabu Bingwa Afrika msimu ujao baada ya kuifungia timu yake bao la pili na la 19 kwake.

Kwa matokeo hayo Geita Gold inaungana na Mtibwa Sugar kushuka daraja hadi la kwanza (Championship) huku timu za Tabora United na JKT Tanzania zitalazimika kucheza mechi za mchujo 'Play off' na timu za daraja la kwanza ili kujaribu bahati yao ya kubaki Ligi Kuu ya NBC.

## Hatimaye Shime amwita Clara Twiga Stars




**BAADA ya kutomwita kwa muda mrefu, hatimaye Kocha Bakari Nyundo Shime amemjumuisha mshambuliaji wa Al Nasr ya Saudi Arabia, Clara Luvanga katika kikosi cha wachezaji 22 cha timu ya taifa ya wanawake, Twiga Stars, kwa ajili ya michezo ya kirafiki dhidi ya Mali na Sudan wiki ijayo. Pichani ni Clara akiwa na Christian Ronaldo wa Al Nassrw .**

## Biashara mguu mmoja ndani kurejea Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Biashara United imefuzu hatua ya mwisho ya mchujo wa kuwania kupanda Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara baada ya kuitoa Mbeya Kwanza kufuatia kuichapa 2-0 juzi Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara.

Mabao ya Biashara United yalifungwa na Charles Lukindo na Abeid Athumani na kwa matokeo hayo Biashara United inafuzu kwa ushindi wa jumla wa 4-0 kufuatia kuichapa Mbeya Kwanza 2-0 kwenye mchezo wa kwanza Uwanja wa Karume mjini Musoma.

Biashara sasa ilikuwa inasubiri timu itakayoporomoka kutoka Ligi Kuu jana zikutane katika mechi mbili za nyumbani na ugenini na mshindi wa jumla ndiye atacheza Ligi Kuu msimu ujao na atakayefungwa atacheza Championship.

